

**CHANGAMOTO ZA KUTAFSIRI *CONSTITUTION OF KENYA 2010* –  
MKINZANO WA KIISIMU NA USAWIDI WA KISHERIA: KIFANI CHA SURA  
YA 3 NA SURA YA 4**

**NA**

**GRACE MWETI**

**C50/80496/2015**

**TASNIFU HII IMETOLEWA KWA MADHUMUNI YA KUTOSHELEZA  
BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI (M.A.) KISWAHILI  
KATIKA CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2018**

**IKIRARI**

Tasnifu hii ni kazi yangu asilia na haijawahi kutolewa kwa minajili ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

**Sahihi**

**GRACE MWETI**

**TAREHE**

Tasnifu hii imewasilishwa kwa idhini yetu kama wasimamizi na washauri wa mwanafunzi tulioteuliwa na chuo.

**Sahihi**

**DKT. ZAJA OMBOGA**

**TAREHE**

**Sahihi**

**BW. JOSEPHAT GITONGA**

**TAREHE**

## **TABARUKU**

Kwa wazazi wangu wapendwa, Bw. Josphat Mbai na Bi. Jennifer Mbai kwa kunifunza dhamana ya masomo tangu utotoni na kuwa dira yangu ya maisha kila mara.

Mume wangu mpendwa Tonny Nzamsa kwa kunipa fursa ya kujiendeleza kielimu licha ya kuwa na mtoto mchanga.

Mwanangu Kimberly Maluki kwa kunivumilia wakati wa kuifanya kazi hii.

## **SHUKRANI**

Mwanzo kabisa namshukuru Mola kwa kunijalia na afya na siha njema wakati wa kuifanya kazi hii.

Nawashukuru wahadhiri wote wa idara ya Kiswahili kwa maarifa walionipa.

Nawashukuru wafuatao: Prof. Habwe, Prof. Kineene, Prof. Mbatia, Dkt. Mbuthia, Prof.

Iribe Mwangi, Dkt. Zaja na Dkt. Jefwa.

Shukrani zangu za dhati ziwaendee wasimamizi wangu Dkt. Zaja na Bw. Gitonga. Walinipa ushauri na mwongozo ulioniwezesha kutimiza ndoto yangu.

Pia nawashukuru wanafunzi wenzangu kwa ushirikiano waliokuwa nao katika safari hii ndefu.

Mwisho shukrani zangu ziendee familia yangu kwa kunihimiza na kunivumilia hata niliposhindwa kuwaamkua nyumbani kutokana na mahitaji ya masomo yangu. Namshukuru mume wangu kwa moyo wa dhati kwa yote aliyonitendea nilipokuwa katika harakati za masomo haya. Mlinihimiza na kuniombea siku zote.

## YALIYOMO

<b>IKIRARI .....</b>	<b>ii</b>
<b>TABARUKU.....</b>	<b>iii</b>
<b>SHUKRANI.....</b>	<b>iv</b>
<b>YALIYOMO.....</b>	<b>v</b>
<b>IKISIRI .....</b>	<b>vii</b>
<b>UFAFANUZI WA ISTILAHI NA VIFUPISHO .....</b>	<b>viii</b>
<b>SURA YA KWANZA: UTANGULIZI .....</b>	<b>1</b>
1.1 Usuli wa Mada .....	1
1.2 Tatizo la Utafiti .....	4
1.3 Maswali ya Utafiti.....	6
1.4 Malengo ya Utafiti .....	6
1.5 Sababu ya Kuchagua Mada Hii.....	6
1.6 Upeo na Mipaka .....	9
1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii.....	10
1.8 Msingi wa Nadharia .....	13
1.8.1 Mihimili mikuu ya nadharia ya <i>Skopos</i> .....	14
1.9 Mbinu za Utafiti .....	17
<b>SURA YA PILI: WASIFU WA SAJILI YA SHERIA NA CHANGAMOTO KATIKA KUTAFSIRI SHERIA.....</b>	<b>18</b>
2.0 Utangulizi .....	18
2.1 Wasifu wa Sajili ya Sheria .....	18
2.2 Wasifu wa Katiba kama Matini ya Kisheria .....	23
2.3 Usawidi wa Kisheria .....	28
2.4 Changamoto katika Kutafsiri kwa Kuegemea Usawidi wa Kisheria .....	31
2.5 Jinsi ya Kukabiliana na Changamoto Zinazojitokeza katika Kutafsiri Sheria .....	35
2.6 Hitimisho.....	36
<b>SURA YA TATU: TATHMINI YA SURA YA 3 YA <i>CONSTITUTION OF KENYA</i> 2010.....</b>	<b>37</b>
3.0 Utangulizi .....	37
3.1 Ufafanuzi wa Sura ya 3 .....	37

3.2 Ukinzani wa Maana Unaojitokeza katika Kutafsiri Sura ya 3 ya <i>Constitution of Kenya 2010</i> .....	37
3.3 Hitimisho.....	45
<b>SURA YA NNE: TATHMINI YA SURA YA 4 YA <i>CONSTITUTION OF KENYA 2010</i></b> .....	<b>46</b>
4.0 Utangulizi .....	46
4.1 Ufafanuzi wa Sura ya 4 ya <i>Constitution of Kenya 2010</i> .....	46
4.2 Ukinzani wa Maana Unaojitokeza katika Kutafsiri Sura ya 4 ya <i>Constitution of Kenya 2010</i> .....	46
4.3 Sababu Zinazochangia Kutokea kwa Ukinzani wa Maana Kisheria Katiba Iipotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili .....	57
4.4 Athari za Tafsiri Potovu kwa Watekelezaji wa Katiba .....	60
4.5 Mbinu Mwafaka Zinazoweza Kutumika Kutatua Ukinzani wa Maana.....	61
<b>SURA YA TANO: MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO .....</b>	<b>64</b>
5.0 Utangulizi .....	64
5.1 Mafanikio, Maoni na Mapendekezo.....	65
<b>MAREJELEO .....</b>	<b>67</b>

## IKISIRI

Utafiti huu unahusu changamoto za kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* kwa kuangazia ulinganifu wa maana unaoibushwa na mikinzano ya kiisimu na kwa njia hiyo kukinza uibukaji wa maana ya kisheria kwa mujibu wa uzingatiaji wa kanuni na matarajio ya usawidi wa kisheria. Kuwepo kwa makosa, hasa utohakika wa maana, unaotokana na tafsiri inayoibushwa katika *Constitution of Kenya 2010* kunakisiwa kulichangiwa na matumizi ya mitazamo na mikakati banifu iliyoegemezwa tu katika usahihi wa kiisimu na kupembeza ulazima wa kusawazisha usahihi wa kiisimu na ufaafu wa usawidi wa kisheria. Uhalisi huu unaojitokeza katika kazi lengwa yaani, tafsiri ya *Constitution of Kenya 2010* ulichochea haja ya kuhitajika kwa utafiti ili kubaini changamoto zinazojitokeza katika kuitafsiri Katiba kama matini ya kisheria. Malengo ya utafiti yalikuwa kuonyesha utohakika na ukinzani wa maana unaojitokeza katika kutafsiri dhana, kauli na istilahi za kisheria kutoka Kiingereza hadi Kiswahili, hasa kwa kuangazia tafsiri ya Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010*. Utafiti huu unatathmini sababu zilizochangia kutokea kwa utohakika na ukinzani wa maana katika tafsiri ya Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010*, kuchanganua athari zake kwa wapokezi wa Katiba hii katika lugha ya Kiswahili na kupendekeza mbinu mwafaka za kutatua ukinzani huu. Data iliyotumika kufanya uchanganuzi wa masuala ya tafsiri ilitolewa kutoka kwenye Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010*. Uchanganuzi uliofanywa kubaini utohakika na ukinzani wa ulinganifu wa maana uliegemezwa katika misingi ya nadharia ya Skopos, hasa kwa kuzingatia kipengele cha nadharia hii kinachosisitiza uamili wa matokeo ya tafsiri yoyote ile, zikijumuishwa tafsiri za matini za kisheria. Matokeo ya utafiti huu yalionyesha kuwa kulikuwa na ukinzani wa kimaana uliojitokeza katika sura hizi. Pia utafiti huu ulibaini kwamba uwepo na utohakika wa maana na ukinzani wa maana ni matokeo ya matumizi ya uelewa potofu na mbinu ambazo hazikusawazisha madai ya kiisimu na madai ya usawidi wa kisheria.

## UFAFANUZI WA ISTILAHU NA VIFUPISHO

- Uraia - Hii ni hali ya mtu kutambulika chini ya sheria kama mwananchi mwenye haki zote katika nchi fulani. Mtu huyo pengine anaweza kuwa raia wa nchi zaidi ya moja.
- Raia - Mtu mwenye haki kisheria kwa sababu ya kuzaliwa au kujisajilisha katika taifa fulani na anayeweza kushiriki katika shughuli zote za taifa hilo.
- Utaifa - Mambo yanayowaunganisha watu kuwa taifa moja.
- Bunge - Baraza la kitaifa linalohusika katika kutunga sheria na pia ni mojawapo ya mihimili mitatu inayounda mfumo wa utawala. Mihimili mingine ni mahakama na serikali.
- Katiba - Jumla ya kanuni ambazo huiwezesha serikali itawale.
- Kifungu - Ibara mojawapo ya matini ya sheria, Katiba au mkataba.
- Ibara - Kifungu cha maneno yaliyokamilika katika matini ya kisheria.
- Sheria - Ni mfumo wa kanuni ambazo kwa kawaida hutekelezwa kupitia taasisi maalum.
- Mahakama- Ni mfumo wa wataalamu na kamati maalumu ambao unatafsiri na kutumia sheria. Mahakama inatoa pia mfumo wa kutatua migogoro.
- Hadhi - Cheo au daraja
- Jinai - Kosa la uhalifu.
- Haki - Uendeshaji wa jambo kufuatia sheria au kanuni zilizowekwa.
- MC - Matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*).
- ML - Matini lengwa (*Katiba ya Kenya 2010*).



## SURA YA KWANZA

### UTANGULIZI

#### 1.1 Usuli wa Mada

Historia kuhusu tafsiri za kisheria katika lugha ya Kiswahili ni finyu sana na ingawaje tafsiri imeendelea kukua kadri muda unavyoendelea kumeanza kuibuka haja na dharura za kutafsiriwa kwa stakabadhi za kisheria za aina mbalimbali. Kulingana na Hilf (1973, kama alivyonukuliwa katika Soriano Barabino, 2006), matini ya kwanza ambayo inaeleza kuhusu kutafsiriwa matini za kisheria ilitokea mwaka wa 1271 (kabla ya Yesu Kristo) huko Misri kupitia kwa tafsiri iliyofanywa kuhusu mkataba wa amani kati ya Wamisri na kiongozi wao Hattusili. (Egyptian-Hittite peace treaty). Mwanzoni kwa sababu watu walikuwa hawajasoma, tafsiri zilizofanywa zililenga mikataba kuhusu mambo ya kawaida yaliyojitokeza kama mikataba ya amani. Maswala yanayoelezea sheria kama inavyoeleweka hii leo hayakuwa yamejitokeza sana. Hatua kubwa katika tafsiri za kisheria ilitokea wakati tafsiri ya *Corpus Iuris Civilis* yake mfalme Justinian ilipofanywa kutoka lugha ya Kilatini hadi Kigiriki katika karne ya sita. Kati ya karne ya saba na karne ya kumi na tatu, tafsiri katika mataifa ya Kiarabu ilijitokeza sana huku kazi nyingi hata za kisheria zikitafsiriwa. Nchi zilipoendelea kuna mambo mengi yaliyojitokeza kuhusiana na tafsiri za kisheria hasa kwa sababu ya maendeleo ya kiteknolojia. Jinsi mambo ya kiutawala yalivyozidi kukua na idadi ya watu kuongezeka basi watu wakaanza kuweka kumbukumbu za kuzaliwa, vifo na hata ndoa. Hii iliongeza idadi ya kazi za kisheria zilizohitaji kutafsiriwa. Tafiti za tafsiri za kisheria kabla ya karne ya ishirini zilikuwa chache ingawaje zimezidi kuongezeka katika karne ya ishirini na moja.

Kulingana na Sarcevic (1997), mwanzoni watafsiri walilazimishwa kutafsiri moja kwa moja katika misingi ya ulinganifu wa neno kwa neno au maana kwa maana ingawaje baadaye haya yalibadilika na tafsiri zikaanza kufanywa kwa njia ya kiufundi kwa kuzingatia madai na wasifu wa taaluma mahususi. Vizuizi hivi vya zamani havikuwa na mchango wowote kwa tafiti za kiusomi zilizofanywa kuhusu tafsiri kwani hazikuzingatia ujumbe katika matini chanzi kikamilifu. Nord (1997) anasema kuwa tafsiri imebadilika sana na imekuwa muhimu kuzingatia yaliyomo katika matini chanzi kuhakikisha kuwa yamehawilishwa katika matini lengwa na wala si kutafsiri maneno tu bila kuzingatia muktadha wa matini ilikoandikwa, muktadha wa matini tafsiri itakapotumiwa na zaidi

lengo na nia ya tafsiri mahususi. Tafsiri kwa miaka mingi ilifanywa kwa kulenga mambo ya kiisimu. Haya yaliendelea hadi wakati ambapo kuliibuka nadharia ya *Skopos* (1980). Kwa miaka mingi, mijadala ya kiusomi iliyotathmini nafasi na umuhimu wa watafsiri katika mchakato wa kutafsiri, iliwachukulia watafsiri kama watu walioshika nafasi za pembeni katika kuhawilisha ujumbe kutoka kwa mwandishi wa matini chanzi hadi msomaji wa matini lengwa. Mawazo haya hatimaye yalibadilika baadaye na mtafsiri sasa anachukuliwa kama sehemu muhimu katika mchakato mzima wa uhawilishaji wa tafsiri. Katika utekelezaji wake wa tafsiri, mtafsiri hana budi kuijua kwa kina hadhira ambayo inalengwa na hivyo basi anaelewa lugha ambayo inahitajika kutumiwa ili ujumbe ufikie hadhira lengwa ipasavyo. Schaffner (1998) anasema kuwa katika maeneo mengi watafsiri hawapewi heshima kama wataalam na viungo vya kimsingi katika mawasiliano yanayokita kuwili. Kuna wale wanaochukulia tafsiri kama njia ya ufundishaji lugha. Kwa mfano kuna utafiti uliofanywa kati ya wanafunzi wanaosomea shahada ya sheria na wale wanaosomea tafsiri huku wakifanya kazi pamoja na ikagunduliwa kwamba watafsiri wana umuhimu sana kwani waliwasaidia wale wa sheria kuelewa hoja muhimu (Way 2002).

Kutafsiri sheria hata hivyo ni mchakato ambao unahitaji ustadi wa hali ya juu ili kupata tafsiri mwafaka ya matini lengwa ambayo inashabihiana sana na matini chanzi kwa misingi ya kuafikia uandishi na uamili wa kisheria. Martin Weston anasema kuwa changamoto katika kutafsiri matini za kisheria huchangiwa na ukosefu wa istilahi mwafaka za kisheria. Lugha ya kisheria ina upekee wake na tafsiri mwafaka lazima ifanyike ili kuonyesha upekee huo na kudumisha matini lengwa kama ya kisheria. Changamoto nyingi katika kutafsiri matini za kisheria hujitokeza hasa kutokana na sababu nyingi kukiwemo na sababu za tofauti za tamaduni za jamii lengwa na pia taasisi zinazolengwa (Weston 1991). Pia anaeleza kuwa wanaotafsiri matini za kisheria wanatarajiwa kuzungumza kwa ufasaha lugha chanzi na lugha lengwa ya tafsiri hiyo na waelewe sheria na mfumo mzima wa sheria ya nchi hiyo. Sarcevic (1997) anaeleza kuwa mtafsiri wa sheria ni lazima awe na ufahamu wa somo hilo kwa kina kando na kuwa na ustadi wa kutafsiri. Uelewa wa istilahi za kisheria ni muhimu na ni sharti mtafsiri awe na ufahamu wa jinsi ya kutatua matatizo ya kisheria, kuchambua makala ya kisheria na pia aweze kuwa na uwezo wa kutabiri jinsi makala hayo yatatekelezwa katika miktadha

tofauti kama vile kortini (Sarcevic 1997:113). Kulingana naye mtafsiri akiwa bora basi hakuna mkinzano wa maana utakaojitokeza katika kutafsiri makala ya kisheria.

Newmark (1988:151) anasema kuwa kutafsiri sheria kunahitaji mwelekeo tofauti kulingana na changamoto zilizopo na ambazo ni tofauti na zile zinazokumba tafsiri za kawaida. Tafsiri za kipekee zimegawanywa katika makundi mawili: tafsiri za kitaaluma na tafsiri za kitaasisi. Tafsiri za kitaaluma ni zile ambazo istilahi zake hazifungwi na utamaduni wa eneo fulani na hivyo ni bia ilhali tafsiri za taasisi ni zile ambazo zinaeleweka tu na jamii mahususi pekee. Tafsiri za kisheria ni za kipekee, hutegemea jamii mahususi na kwa hivyo ni jukumu la mtafsiri kuwa mwaminifu kwa toni iliyotumika, afuate mpangilio wa matini chanzi na kwa wakati huohuo ahakikishe ujumbe unamfikia msomaji kwa njia ya wazi na inayoeleweka bila kuwa na uhuru wowote kwani hili halikubaliki katika kutafsiri sheria. Pommer (2008) anaongezea kuwa tafsiri za kisheria huwa hazipo katika ombwe tupu la utamaduni na hili lisipozingatiwa huwa ndio mwanzo wa matatizo yote katika tafsiri za kisheria (Pommer 2008:360). Kwa hivyo mtafsiri ni lazima azingatie utamaduni wa jamii husika wakati wa kufanya tafsiri yake ili kutumia istilahi au maneno yaliyo na maana inayoeleweka na jamii ile na ambayo yanaafiki muktadha.

Kulingana na Toury (1995) kutafsiri ni mchakato ambao ni mgumu sana na changamano na unahitaji mtafsiri atumie ujuzi wake wa kiusomi ili kuwa na tafsiri bora. Mtafsiri pia inahitaji atumie akili ili kuelewa mambo ya kawaida yanayoelezwa. Katika tafsiri kuna maswala muhimu ambayo yatahitaji mtafsiri kutumia uelewa wake kuhusu istilahi zilizotumika na ambazo zinaweza kuwa na maana ya ndani zaidi. Kwa mfano katika muktadha wa jamii ya Kenya, wakati wa kutafsiri makala inayohusu ufisadi mtafsiri anapokumbana na neno kama ‘chai’ anafaa kuelewa kuwa maana iliyokusudiwa hapa ni hongo na wala tafsiri yake si ‘tea’ kwa Kiingereza. Vilevile, mtafsiri anafaa kuwa na uelewa wa maswala ibuka katika jamii na hasa yanayohusu teknolojia.

Matatizo katika tafsiri yanaweza kutatuliwa kwa kutumia nadharia iliyoasisiwa na Nida ya usawe-dhima. Newmark (2005: 83) anaeleza usawe-dhima kama utaratibu unaochukua nafasi kubwa kati ya matini chanzi na matini lengwa na kwamba nadharia hii inafaa sana katika tafsiri hata tafsiri za kisheria. Sarcevic (1988: 964; 1989: 278-279) anaeleza usawe

dhima wa kisheria kama istilahi katika sheria ambapo mawazo yaliyomo katika matini lengwa ya kisheria huwa na dhima sawa na yale yaliyo katika matini chanzi. Weston (1991:23) naye kwa maoni yake anaeleza kuwa huu ndio mfumo mwafaka wa kutafsiri. Nida (2001) anasema kuwa ‘usawe dhima’ huwa na tafsiri ambazo zinafaa zaidi kwani hakuna tafsiri ambayo ina matini chanzi inayolingana kabisa na matini lengwa.

Licha ya changamoto za kijumla kuhusu tafsiri za kisheria kuna wataalam mbalimbali wanaoangazia matini za kisheria. Sakavera (2001) katika makala *Difficulties and some Problems in Translating Legal Documents* anaeleza matatizo ambayo hujitokeza katika kutafsiri matini za kisheria. Baadhi ya changamoto hizi ni kama vile ukosefu wa ulinganifu wa istilahi na utoshelevu katika matini za kisheria na matatizo katika kuhamisha mawazo kutoka utamaduni wa mwandishi hadi utamaduni wa mpokeaji. Changamoto hutokea pia katika kutafsiri kutoka kwa mfumo mmoja wa kisheria hadi mwingine. Katika makala haya pia anaelezea kuhusu sifa mahususi za matini za kisheria na lugha ya sheria kwa jumla. Cao (2007) naye amezungumzia kuhusu lugha ya kisheria na akaeleza sifa bainifu za sajili ya sheria. Ameainisha matini za kisheria kwa njia mbalimbali na akaonyesha matatizo ya uainishaji huo. Amefafanua chanzo cha matatizo ya kutafsiri sheria katika viwango mbalimbali vya kiisimu.

Kazi ambazo zimejitokeza kuhusu matini za kisheria zinaangazia sana matatizo au changamoto katika kutafsiri matini za kisheria. Kazi hizi pia zinaangazia maswala yanayofungamana na dhana ya kiisimu na hazidadisi kuwa kuna matapo ya kisheria yaliyopuuzwa. Licha ya tafiti za kijumla kufanywa kuhusu makala ya kisheria, kuna mwanya unaojitokeza unaohusiana na ushirikishwaji wa usawidi wa kisheria katika kutafsiri makala ya kisheria. Utafiti tulioufanya ulionyesha baadhi ya changamoto hizi na jinsi zinavyoweza kutatuliwa.

## **1.2 Tatizo la Utafiti**

Utafiti huu ulilenga kuonyesha kuwepo kwa changamoto za kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* zinazohusiana na ujitokezaji wa kimikinzano ya kimaana katika misingi ya kiisimu na misingi ya kisheria. Utafiti huu ulichochea na uelewa wetu kwamba japo tafsiri za kisheria zimewahi kushughulikiwa katika lugha ya Kiswahili, tafsiri ya Katiba ni upeo mpya unaoibuka na unaojikita katika eneo la tafsiri tekelezi au tafsiri amilifu.

Hapana shaka kwamba tafsiri ya Katiba ina upekee wa aina maalum unaokita katika kutambua masuala ya kiisimu na ya kisawidi cha kisheria ambayo yamewekezwa katika Katiba. Kuna haja ya kuelewa mahusiano yaliyoko katika tafsiri nzuri na matekelezo ya Katiba. Lugha ya Kiswahili kikatiba imekubalika na kupewa kipaumbele kama lugha rasmi ya kitaifa na kutambuliwa na kuingizwa masharti na maelekezi ya kikatiba ya ushiriki na ushirikishwaji wa wananchi katika michakato ya utoaji maamuzi, matumizi ya Kiswahili kama mkakati wa kutafakari masuala nyeti ya kijamii, kama njia ya kuangazia matekelezo ya kanuni na dhana za kisheria na kama njia ya kutafakari michakato ya mitagusano ya kijamii. Kwa sababu hizi, utafiti huu ulinuia kubaini nichangamoto zipi zinazojitokeza na kuzua mkinzano wa maana katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* na ni nini athari ya mkinzano huu katika matekelezo ya kisheria na Katiba hii. Ni muhimu pia kujaribu kuelewa na kuonyesha kama tafsiri ya Katiba inatumiwa kama mbinu mahususi ya kuwasilisha jumbe za aina maalum za kisheria inapozingatiwa kwamba jumbe zinazowasilishwa kwa mitazamo ya kisheria zinaweza kukiuka ukawaida wa lugha lakini kwa nia ya kuwasilisha uelewa fulani wa kisheria.

Changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* hutokana na mkinzano ya dhana na istilahi. Istilahi za kisheria zimekuwa zikiundwa lakini kuna matatizo anuwai ambayo yamesababisha kutokuwepo na mafanikio yanayoridhisha. Matatizo haya yamesababisha upungufu mkubwa wa istilahi na mparaganyiko wa baadhi ya istilahi unaosababishwa na misingi potofu ya uundaji wa istilahi (Mwansoko pamoja na wengine; 1992:22). Katika kutafsiri matini za kisheria ukosefu wa istilahi mwafaka za kutumika huchangia kutokea kwa mkinzano wa maana. Kutafsiriwa kwa anwani za vifungu vya *Constitution of Kenya 2010* na undani wa tafsiri katika vifungu hivyo kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kwenye *Constitution of Kenya 2010* unadhihirisha uwepo wa maana za kiisimu ambazo zinakisiwa kushawishiwa na tafsiri za kikamusi na kwa njia hii kusababisha kubana maana za kisheria zinazojitokeza katika matini lengwa.

### 1.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kujibu maswali yafuatayo:

- i) Je changamoto za kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* zinazohusiana na ujitokezaji wa mikinzano ya kimaana katika misingi ya kiisimu na misingi ya kisheria ni zipi?
- ii) je ni sababu gani zinazochoea kutokea kwa ukinzani huo?
- iii) je ukinzani huu wa kimaana unaathiri vipi upokezi na uelewa wa Katiba katika miktadha lengwa?
- iv) je kuna mbinu mwafaka kuelewa ukinzani huu?

### 1.4 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu unalenga kufikia madhumuni yafuatayo:

- i) kuonyesha changamoto za kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* zinazohusiana na ujitokezaji wa mikinzano ya kimaana katika misingi kiisimu na misingi ya kisheria,
- ii) kubaini sababu zinazochoea kutokea kwa ukinzani wa huo,
- iii) kubaini jinsi ukinzani wa kimaana unavyoathiri upokezi na uelewa wa Katiba katika miktadha lengwa,
- iv) kubaini mbinu mwafaka za kuelewa ukinzani huu.

### 1.5 Sababu ya Kuchagua Mada Hii

Nchini Kenya Kiswahili ni lugha inayotumika kama njia ya mawasiliano na wananchi wengi. *Katiba ya Kenya 2010* katika Sura ya 2, Kifungu cha 7 katika ibara ya (i-ii) inapoelezea kuhusu lugha na njia za mawasiliano inafafanua kuwa; lugha ya taifa ni Kiswahili na lugha rasmi za Kenya ni Kiswahili na Kiingereza. Hii inamaanisha kwamba lugha ya Kiswahili ina hadhi ya juu zaidi kuliko lugha ya Kiingereza ambayo ililetwa na wakoloni yaani Waingereza. Hivyo basi kutafsiri Katiba katika lugha ya Kiswahili ni jambo ambalo linashinikizwa na sababu za kikatiba na kitaifa ili kuwezesha watu wengi wapate yaliyomo katika Katiba yakijumuisha dhana, kanuni, maadili, wajibu, maelezo na maelekezi ya kikatiba bila shida, utata au kuchanganyikiwa kwa aina yoyote. Katiba ni stakabadhi muhimu inayoweka mkataba

kati ya watawaliwa na kutoa maelezo na maelekezi kuhusiana na wajibu na majukumu ya kikatiba ya kila mwananchi kwa jamii.

Katika Sura ya 4, Kifungu cha 35 katika ibara ya i-iii, *Katiba ya Kenya 2010* inazungumzia haki, uhuru na haja ya kikatiba ya ufikiaji na upataji habari kwa kutaja na kueleza kuwa;

**Kielelezo 1;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<p>(1) Every citizen has the right of access to-</p> <p>(a) Information held by the State; and</p> <p>(b) Information held by any another person and required for the exercise or protection of any right or fundamental freedom.</p> <p>(2) Every person has the right to the correction or deletion of untrue or misleading information that affects the person.</p> <p>(3) The State shall publish and publicise any important information affecting the nation.</p>	<p>(1) Kila mwananchi anayo haki ya kupata-</p> <p>(a) Habari ilizonazo Serikali</p> <p>(b) Habari zozote zilizo na mtu mwingine na zinazohitajika ili kutekeleza au kulinda haki yoyote au uhuru wowote wa kimsingi.</p> <p>(2) Kila mtu anayo haki ya kutaka kurekebisha au kubatilishwa kwa habari zozote za uongo au za kupotosha zinazomhusu mtu huyo.</p> <p>(3) Serikali itachapisha na kutangaza kila habari inayohusu taifa.</p>

Kifungu hiki kinaonyesha kuwa mwananchi ana haki ya kupata habari kutoka kwa Serikali. Katiba kama matini ya kisheria hivyo basi haifai kuwa na ukinzani wowote ambao unaweza kuathiri uwasilishaji wa ujumbe kwa wananchi.

Baadhi ya wataalam katika nyanja ya mawasiliano wamehoji kwamba mawasiliano ya aina yoyote ile yanaweza kukumbwa na vizuizi vya aina nyingi, vile vilivyomo ndani ya lugha na vile vilivyo nje ya lugha. Kwa mfano, Nijikamp (na wengine 1990) anatoa kauli kwamba baadhi ya vizuizi vya mawasiliano vilivyo nje ya lugha ni pamoja na vizuizi vya kitamaduni, kilugha, kisheria au kitaasisi. Kwa upande mwingine kuna vizuizi vya kimawasiliano vinavyohusiana na wasifu, ufundi na taratibu za kitaalam za lugha ya sajili mahususi, kama vile sajili ya kisheria. Hii ina maana kwamba ikiwa watekelezaji wa sheria, kwa mfano, wafasiri wa matini za kisheria hawana udhibiti wa kijumla na udhibiti

wa kiufundi wa lugha kisheria wanaweza sio tu kuibua utata na ukinzani wa maana za kisheria, bali pia kutatiza au kuzuia mawasiliano ya kisheria. Uhalisi huu unajibainisha kwa maana kuwa, licha ya *Constitution of Kenya 2010*, katika Kifungu cha 35 kutoa maelezo na maelekezi kuhusiana na uhuru na haki ya ufikiaji na upataji habari kwa kila mwananchi, ukweli ni kwamba si kila mwananchi ana uwezo wa kuifikia habari au kuipata habari ya kisheria, kwa sababu ya kizingiti kimoja, ukosefu wa udhibiti na umaizi wa lugha ya kisheria. Njia moja ya kukabiliana na kizingiti hiki kwa uhalisi wa nchi ya Kenya, inahusiana na haja na dharura iliyoko ya kutafsiri Katiba kutoka Kiingereza hadi Kiswahili ili kuwezesha umma mpana zaidi kuzifikia, kuzielewa na kuzitumia habari za kisheria.

Kutafsiri Katiba kunahitaji weledi, utalam na umakinifu unaodhihirisha uelewa wa wasifu, ufundi na matumizi sio tu ya istilahi za kisheria bali mfumo mzima wa lugha ya kisheria inayoafiki vitengo mahususi vya kisheria na taratibu za kisheria zinazofaa ili kuhakikisha ujumbe mpana wa kisheria ulioko katika Katiba haujapotoka. Ili kufikia hili lazima mtafsiri ahakikishe kuwa amewajibika kwa njia nyingi kuanzia kuwajibikia matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*), kuwajibikia upekee wa lugha ya kisheria hususan taratibu zake za kiuandishi kama vile usawidi wa kisheria na, hatimaye kuwajibikia wapokezi wa tafsiri kwa maana ya kumwezesha mwananchi kupata habari amilifu zinazofaa. Mbali na matarajio haya, kuna matarajio mengine ya ziada ya uwajibikaji, kama anavyohoji Cao (2014) kuwa maadili ni muhimu kwa mtafsiri wa makala ya kisheria, kwamba hana budi kuhakikisha amewajibika kuipa hadhira yake ujumbe bila kuupotosha. Kanuni, maelezo na maelekezi ya kikatiba kuhusiana na haki na uhuru wa mwananchi kupata habari au nakala rasmi za kisheria zinazoeleweka, hayawezi kuafikiwa pale ambapo kuna ithibati kwamba stakabadhi rasmi zilizotafsiriwa, kama vile *Constitution of Kenya 2010*, zina walakini, dosari na mapungufu ya aina nyingi. Hili ni jambo muhimu lilitupelekea kuchagua mada inayohusiana na changamoto za kimaana na uelewa zinazojibainisha katika *Katiba ya Kenya 2010*. Kauli ya awali ya utafiti huu inahoji kwamba tafsiri bora na amilifu ya Katiba pia itawezesha utekelezaji athirifu wa sheria katika miktadha mbalimbali kama vile katika maamuzi ya kesi zinazohusiana na ukiukwaji wa sheria za uraia na haki zinazozungumziwa katika Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Katiba ya Kenya 2010*.



Tunaangazia Sura ya 3 inayohusu Uraia na Sura ya 4 inayohusu Sheria ya Haki katika *Constitution of Kenya 2010*. Uraia ni dhana ya kimsingi katika Katiba ambayo inahitaji sio tu kudumishwa bali pia kulindwa na kutetewa, ni dhana inayohitaji kuimarishwa na kudhibitiwa kwa njia ya kisheria. Kwa hivyo, ipo haja kwa kila raia kuelewa anavyowajibikiwa kikatiba na anavyoiwajibikia Katiba kama vile ulazima ulioko kutii sheria za nchi yake. Anahitaji kuelewa ana haki na majukumu ya kisheria kuhusiana na haki katika nchi, kuelewa misingi na falsafa inayohusiana na utetezi wa haki na hivyo basi kuepuka utata wowote wa uelewa unaotokana na usawa wa haki kwa wananchi wote. Mada hizi ni muhimu sana kwani ni lazima mtu kujua haki zake kuhusu uhalali wake kuhusu anapoishi. Sura hizi mbili zinaingiliana kwani ukijua sheria kuhusu uraia wa nchi ya Kenya na ukawa mkazi basi itabidi ufahamu sheria ya haki kama raia wa nchi hiyo ili haki zako zisije zikakiukwa.

### **1.6 Upeo na Mipaka**

Katika utafiti huu tulilenga kuonyesha uwepo wa mikinzano, upotoshi na upoteaji wa maana, hususan maana ya kisheria katika tafsiri za matini ya kisheria. Katika misingi ya ubainishaji huo tulilenga kuonyesha sababu zinazosababisha mikinzano ya kimaana wakati matini lengwa ya kisheria (*Katiba ya Kenya 2010*) inapolinganishwa na matini chanzi ya kisheria (*Constitution of Kenya 2010*). Tulijikita katika Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Katiba ya Kenya (2010)*. Sura ya 3 ina vifungu saba (12-18) nayo Sura ya 4 ikiwa imegawika katika vifungu arobaini na moja (19-59). Sura ya 3 inazungumzia kuhusu uraia na Sura ya 4 inazungumzia sheria ya haki.

Katika utafiti wetu tulilenga Katiba ya sasa ambayo ni *Constitution of Kenya 2010*. Katiba hii ilichukua nafasi ya Katiba ya wakati wa uhuru mwaka wa 1963. Mwanasheria Mkuu wa Kenya alikabidhiwa Katiba hii mpya na baadaye ikafanyiwa kura ya maoni tarehe 4 Agosti 2010. Mojawapo ya sababu za kubadilisha Katiba hii ilikuwa ni kuongeza vipengele muhimu ili kuwafaidi wananchi zaidi. Baadhi ya vipengele vilivyoongezwa ni orodha ya haki inayotambua haki za jamii katika Sura ya 3 ambayo ndiyo mojawapo ya sura ambazo tumelenga katika utafiti wetu. Pia katika Katiba hii Sura ya 11 inayohusu ugatuzi iliongezwa.

Utafiti huu ulitumia lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Hii ni kwa sababu matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*) ambayo tulitumia imeandikwa kwa lugha ya Kiingereza na kisha ikatafsiriwa hadi Kiswahili. Kiswahili pia ni lugha ambayo imetambulika kama lugha rasmi ya kitaifa katika nchi ya Kenya na kinatumika na wengi katika mawasiliano. Hivyo basi kutafsiri Katiba hadi Kiswahili ilibidi kutafsiriwa kwa sababu wananchi wengi huelewa Kiswahili. Ingawaje utafiti wetu ulinuiwa kuchunguza kama kweli ujumbe ulio katika Katiba ya Kiingereza (*Constitution of Kenya 2010*) umewasilishwa ilivyo katika tafsiri yake ya Kiswahili (*Katiba ya Kenya 2010*) kwa kulenga kuchanganua ni kwa kiasi gani tafsiri hii inaakisi usawidi wa kisheria.

Utafiti huu ulilenga kuonyesha mikinzano ya kimaana inayojitokeza Katiba inapotafsiriwa hasa kwa kulenga maana ya kisheria na kuona kama maneno na vifungu vimetafsiriwa vilivyo. Tulichunguza kama maana inayojitokeza katika kutafsiri istilahi za kisheria katika matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*) imedumishwa katika matini lengwa (*Katiba ya Kenya 2010*). Tulichunguza kwa kulenga hasa maneno na vifungu tofauti na kuona kama tafsiri iliyofanywa inaleta ukinzani wa maana. Tuliaweka maneno haya na vifungu hivi katika jedwali kisha kulinganisha MC na ML na kuonyesha kama maana ile ile ya kisheria iliyoko katika MC imedumishwa katika ML.

### **1.7 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada Hii**

Hapana shaka kwamba dhana ya tafsiri za matini za kisheria imewahi kujitokeza na kujadiliwa kwa njia anuwai katika lugha ya Kiswahili na pia katika lugha nyingi za kilimwengu. Tafiti kuhusiana na tafsiri za matini za kisheria zilizokwisha kufanywa katika lugha ya Kiswahili zinatofautiana kwa misingi ya malengo yaliyokusudiwa kutekelezwa. Ufahamu huu unatuchochea kuhoji kwamba mapitio ya maandishi na machapisho yaliyodhamiriwa katika utafiti huu yalilenga kubainisha masuala ibuka katika kazi ambazo zimetafiti na kuliangazia suala la tafsiri za matini za kisheria kwa jumla na katika lugha ya Kiswahili hasa. Hii ni kwa kuwa kazi aina hiyo zilizopo kwa kiasi zitakuwa zinaoana na mada ya utafiti huu na kwa hivyo zitachangia kukuza hoja na kauli zitakazotuelekeza katika mahitimisho jumla. Kwa hivyo, mapitio ya maandishi na machapisho yanayojumuishwa hapa ni mapitio yaliyo na mlandano wa masuala ya kisheria katika miktadha ya tafsiri kama vile wasifu wa lugha ya matini za kisheria, majukumu na matarajio katika kutafsiri matini za kisheria, aina za matini za kisheria,

athari za ukosefu wa ufahamu wa kutafsiri matini za kisheria na masuala mengine sawia na hayo. Mapitio haya yalilenga vilevile kuonyesha ufaafu na umuhimu wa kuzingatia matarajio ya kutafsiri matini za kisheria kama vile kuelewa wasifu na nafasi ya usawidi wa kisheria na mahusiko yake katika tafsiri katika lugha ya Kiswahili, kuonyesha jinsi dhana ya matini ya kisheria inavyotumika kusimba maana za kisheria na kuibua upekee wa kimaana katika miktadha mahususi ya matumizi ya kisheria. Kwa kiasi mapitio haya yaliangazia pia nadharia iliyotumiwa katika utafiti huu ili kuonyesha ufaafu wake katika kulidadisi suala hili la tafsiri za matini ya kisheria.

Lugha ya kisheria imeelezwa kupitia misimamo miwili. Mtazamo wa kwanza ni kwamba hakuna lugha ya kisheria na kama ipo ni sehemu ya lugha ya kawaida na pili ni kuwa lugha ya kisheria ni lugha ya kitaaluma. Mwanafilosofia wa kisheria, Hart (1954), ana tetezi kwamba lugha ya kisheria ni tofauti kabisa na lugha ya kawaida. Hart anasema kwa sababu ya upekee wa lugha ya kisheria basi 'legal language is *sui generis*, kumaanisha kuwa lugha ya kisheria ni ya kipekee. Anasema kuwa istilahi za kitaaluma huathiri maana ya kila neno ambalo limetumika katika muktadha na istilahi za kisheria zina maana mahususi kutegemea muktadha wa mfumo wa sheria uliotumika. Tulitumia hasa madai ya Hart katika uchunguzi wetu ili kubaini kama *Constitution of Kenya 2010* imetafsiriwa kwa njia mwafaka na kufikia viwango vinavyoakisi yaliyomo katika matini chanzi kwa kutumiamikakati inayoweza kufikiwa kwa viwango vya usawidi wa kisheria na kwa njia hiyo kuibusha maana ya kiisimu pasina kupotosha maana mahususi ya kisheria inayokusudiwa na vilevile kuleta maana iliyodhamiriwa kuakisi miktadha mahususi bila kuwa na utata wowote kwa kutegemea muktadha.

Charles Caton (1963) ambaye ni mwanafilosofia wa kiisimu naye anasema kuwa lugha ya kisheria ni ya kitaaluma lakini 'lugha ya kitaaluma ni nyongeza ya lugha ya kawaida' (Carton 1963: viii), inaweza ikawa Kiingereza cha kawaida, Kifaransa cha kawaida au Kiswahili cha kawaida. Anasema kuwa lugha za kitaaluma zina sintaksia sawa na ile ya lugha ya kawaida na vitendo usemi vinavyotekelezwa katika mazungumzo ya kawaida zinaweza kutekelezwa katika muktadha wa kitaaluma na istilahi pekee ndizo zitabadilika.

Harvey (2002:177) anasema kutafsiri sheria ni jambo tata sana na kunahitaji ujuzi maalum, maarifa na uzoefu kwa mtafsiri. Sheria huhitaji usahihi katika kutafsiriwa

kwake na kukiwepo na utata wa aina yoyote basi kutatokea kutoelewana. Utata katika lugha unaotokana na kutojua sheria huleta ugomvi na migogoro katika sheria (Endicott 2000:190). Katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili tulichunguza kama kuna utata unaojitokeza na jinsi unaweza kuathiri utekelezwaji wa Katiba ile. Lugha inafaa kuwa wazi nailiyo sahihi na ukweli wa kauli yoyote katika lugha ama sheria inaweza kuhakikiwa kwa kurejelea muktadha maalum au hali fulani. Kutafsiri istilahi za kisheria pia kunahitaji uelewa wa lugha zote mbili zinazolengwa ndiposa tupate tafsiri bora.

Kulingana na Cao (2007) lugha ya kisheria inaweza kuchukuliwa kama rejista. Rejista ni matumizi ya lugha kutegemea muktadha (Halliday and Hasan (1985:41). Rejista ni kile unachozungumza kwa wakati fulani, kutegemea kile unachofanya na hueleza jinsi lugha hiyo inafaa kutekeleza jambo fulani kwa kutegemea hadhi katika jamii na jinsi watu wanavyotagusana (Halliday 1985). Rejista ya kisheria hufanana sana na lugha ya kawaida. Lugha ya kisheria kamarejista ina matumizi mengi ya lugha ya kitaaluma. Ingawaje lugha hii ina lengo sawa na lugha ya kawaida hatuwezi tukaifananisha moja kwa moja na lugha ya kawaida. Lugha ya sheria hutumika katika maeneo tofauti lakini lugha iliyotumika itategemea muktadha unaolengwa. Kwa mfano lugha inayotumika na mawakili kortini itatofautiana na ile inayotumika katika uandishi wa Katiba. Kulingana na Cao (2007) tafsiri za kisheria zinaweza kugawika katika makundi kwa kufuata mikondo tofauti. Kwanza kwa kutegemea yaliyomo na kuwa na makundi kama vile; tafsiri za makala ya kibinafsi, tafsiri za makala ya kiusomi na tafsiri kuhusu makubaliano ya kitaifa. Lugha ya kisheria huweza kugawa pia kwa kutegemea hali ya matini chanzi. Makundi yanayojitokeza ni yale yanayohusu sheria inayoweza kutekelezwa na ile isiyoweza kutekelezwa kwa mfano inayohusu tafiti za kiusomi.

Kazi ambazo zimejitokeza kuhusu tafsiri za kisheria ni kama vile Kamusi ya Sheria Kiingereza – Kiswahili yake Mlacha S.A.K (1999). Istilahi za kisheria zimeweza kufafanuliwa katika kamusi hii. Ingawaje kamusi husaidia katika uelewa wa maneno tofauti, zinafaa kutumika kwa uangalifu sana hasa katika tafsiri za kisheria ambazo hubidi mtafsiri kuzingatia muktadha ambamo maneno hayo yametumika bila kuzingatia moja kwa moja maana za kikamusi. Hii ni kwa sababu matini za kisheria kama vile

Katiba huwa na matumizi ya maneno ya kawaida ambayo huwa na maana tofauti katika muktadha wa kisheria.

Waithira (2014) alizungumzia changamoto za kutafsiri matini za kisheria kwa kutathmini Sura ya 11 ya *Constitution of Kenya 2010* inayohusu ugatuzi. Alidhihirisha kuwa mtafsiri huweza kukumbana na tatizo la ukosefu wa ulinganifu wa istilahi wakati wa kutafsiri matini za kisheria. Hii ni kwa sababu maana hujitokeza katika misingi ya kiisimu ya kileksia, sintaksia na kisemantiki. Ingawaje yeye alitumia misingi ya kiisimu kinyume na utafiti wetu unaolenga kiwango cha usawidi wa kisheria.

### **1.8 Msingi wa Nadharia**

Katika utafiti huu tuliongozwa na nadharia ya *Skopos* iliyoasisiwa na Hans. J. Vermeer miaka ya 1970 huko Ujerumani. *Skopos* ni neno la Kigiriki ambalo lina maana ya ‘nia’. Kila matini hutolewa ili kutimiza malengo fulani na lazima malengo haya yatimizwe. Nadharia ya *Skopos* inahoji na kutoa kutoa kauli kwamba: si hoja kama tafsiri inawasilishwa kwa njia ya uzungumzaji au kwa maandishi ila kilicho muhimu ni kuhakikisha tafsiri yako inatekeleza majukumu yanayohitajika kutekelezwa na watu wanaoitumia na kwa njia ambayo wanataka itumike. Msingi wa nadharia hii ni kuiona tafsiri kama utekelezaji wa kitendo mahususi kwa kuzingatia uamili wa tafsiri katika miktadha lengwa pasina kuipotisha matini asilia kimaana. Nadharia hii inasisitiza kuwa kila tafsiri hutafsiriwa kwa lengo fulani na lazima litimizwe kwa kadri iwezekanavyo katika miktadha lengwa. Kwa hivyo basi, tafsiri huzalishwa kwa ajili ya hadhira mahususi kwa lengo mahususi na muktadha maalum (Vermeer 1989a). Nadharia hii huonyesha umuhimu wa mtafsiri katika mchakato mzima wa tafsiri kama kiungo ambaye ana mchango mkubwa kuiwezesha tafsiri kutekeleza majukumu mahususi.

Nadharia hii hudhamiria kutathmini matini kwa malengo maalum ambayo yanapelekea kukamilisha dhima sawa katika utamaduni chanzi na utamaduni lengwa. Hivyo kulingana na mkabala huu, tafsiri athirifu ni ile inayowezesha hadhira lengwa kupata tafsiri yenye ushikamani na matini chanzi (Lauscher,2000). Kulingana na Vermeer (1989a) lengo la nadharia ya *Skopos* ni kueleza shughuli ya tafsiri katika mtazamo wa lugha lengwa. Kwa ujumla nadharia hii imejikita katika malengo ya tafsiri ambayo huukilia mbinu na mikakati ya tafsiri inayotumika katika kutoa matokeo stahiki ya kidhima (Nord, 2007).

### **1.8.1 Mihimili mikuu ya nadharia ya Skopos**

Kulingana na Nord (1997, p. 18), mawasiliano hutokea pale ambapo ishara hutolewa kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji. Mawasiliano yanapotokea katika jamii za watu wenye utamaduni sawa huwa hakuna utata kuelewana kwa sababu hali ya msemaji na msikilizaji ni sawa. Msemaji na msikilizaji wakitoka katika tamaduni tofauti hali inabadilika na mtafsiri anahitajika ili kupitisha ujumbe kutoka kwa msemaji hadi kwa msikilizaji. Watafsiri husaidia katika mawasiliano baina ya watu wawili watumiao lugha zinazotofautiana. Nord (1997, p. 35) anasema kuwa tafsiri hufanywa pale inapohitajika kutekeleza jukumu fulani mahususi katika miktadha mahususi. Hili hutokana na maagizo ambayo hutolewa ili kutekeleza tafsiri mahususi yoyote ile. Kulingana na Nord ni lazima maagizo hayo yaeleze kuhusu tafsiri inayotakikana ndiposa mtafsiri ajue nia ya tafsiri yenyewe. Maagizo haya hayafai kumweleza mtafsiri jinsi atakavyofanya kazi yake. Tafsiri bora itategemea mtafsiri na ujuzi wake kuhusiana na taaluma ile na uwezo wake wa kutafsiri.

Mtafsiri huhitajika kuzingatia nia ya tafsiri ili kuwa na tafsiri athirifu. Mtafsiri lazima kwanza aelewe nia ya tafsiri ni gani, kama ni ya kufahamisha kuhusu jambo fulani, kuelimisha au kufurahisha ili aweze kujua jinsi atakavyofanya tafsiri yake. Kuelewa nia ya tafsiri huwa kunamsadia mtafsiri kujua rejista atakayotumia katika kufanya tafsiri ile, maneno atakayoteua, urefu wa sentensi atakazotumia na maelezo mengine kuhusu tafsiri ile. Hii ni kumaanisha kuwa ni lazima pia aelewe kundi linalolengwa ni lipi ili kuwasilisha ujumbe wake ilivyo. Kwa mfano, kauli hizi na hatua hizi zinazopendekezwa na nadharia ya Skopos zinashadidia ukweli kwamba watekelezaji wa tafsiri ya *Constitution of Kenya 2010*, hawakukita uelewa huu kama mwongozo wa utekelezaji wa tafsiri ya Sura ya 3 na Sura ya 4 ya Katiba hii. Kwa kuwa kubaniwa kwa Katiba kuna malengo anuwai tena malengo changamano, mtafsiri hana budi kuelewa nia zilioekezwa katika Katiba yenyewe, kisha kuelewa nia ya kutafsiri Katiba kama matini ya sheria, jambo ambalo litamshurutisha mtafsiri kujua jinsi anavyotakikana kutafsiri ili matini ile isipoteze upekee wake wa kiamili kuwa matini ya kisheria.

Katika utekelezaji wa tafsiri za matini za kisheria, inabidi mtafsiri awe na uelewa mseto wa mambo yatakayofanikisha tafsiri yake. Mambo haya yanajumuisha uelewa wa kijumla wa lugha lengwa, udhibiti wa lugha mahususi ya sajili husika, taratibu za kiuandishi za matini au sajili husika pamoja na taratibu za uekezaji maana katika maneno, istilahi au hata mifumo ya sentensi inayohusika. Haya yatamsaidia mtafsiri kuweza kujua vile anavyotakikana kuwasilisha ujumbe bila kukiuka kanuni na kaida za matini husika na matarajio ya kundi pokezi la matini inayotafsiriwa. Mtafsiri anapotumia lugha inayoafiki kaida zote zinazohusika nainayoeleweka na hadhira lengwa basi matini ile itawiana na matini chanzi kimfumo na kimuundo na kuna uwezekano nia ya kiutekelezi ya tafsiri ile itafikiwa. Kwa mfano katika kutafsiri Katiba ya Kenya mtafsiri inabidi aelee utamaduni wa lugha ya Kiswahili, aelee lugha ya Kiswahili vizuri na pia awe na uelewa wa hadhira inayolengwa.

Matini lengwa huwa haina ujumbe asilimia moja unaofanana na ule katika matini chanzi. Hii ina maana kwamba hakuna tafsiri ambayo haina dosari. Hii ni kwa sababu lugha hutofautiana sana katika mambo mengi kama vile uwepo wa dhana mahususi, msamiati mahususi, istilahi za kipekee, miundo ya maneno na hata miundo ya sentensi. Uhalisi huu una maana kwamba wakati mwingine kupata istilahi mwafaka zinazowiana kimaana katika lugha lugha chanzi na katika lugha lengwa huwa ni vigumu. Hata tukitafsiri tena kutoka matini lengwa hadi matini chanzi huenda maana ikawa tofauti sana. Kwa mfano *the rights of standing* katika misingi ya uelewa wa sheria inaweza ikatafsiriwa kama haki za kulalamika, lakini tukitafsiri kwa Kiingereza tena itakuwa *right to complain*.

Tafsiri ni lazima pia ifuate kanuni ya uwiano kulingana na nadharia ya *Skopos*. Kanuni hii ina maana kuwa matini lengwa lazima iwe na maana kwa hadhira lengwa katika utamaduni wa lugha lengwa na katika muktadha wa kimawasiliano ambao matini lengwa itatumika. Matini lengwa lazima ifuate utaratibu unaofaa na iwiane na matini chanzi ili ujumbe ueleweke vizuri na hadhira lengwa. Kwa mfano katika kutafsiri sheria ni lazima mtafsiri ahakikishe kuwa ujumbe katika MC umewiana na ule katika ML.

Katika kutafsiri kulingana nadharia ya *Skopos* pia ni lazima kanuni ya uaminifu izingatiwe. Kanuni hii ina maana kuwa lazima kuwepo ushikamani wa kimatini baina ya matini lengwa na matini chanzi ambao ni sawa na usahihi wa matini chanzi. Hata kama

nia ndiyo humwongoza mtafsiri katika kufanya tafsiri yake, ni lazima ahakikishe kuwa matini chanzi inashikamana na matini lengwa ili kutowasilisha ujumbe ambao umepotoka kwa hadhira lengwa.

Tulitumia nadharia hii ya *Skopos* kwa sababu ni ya kiutekelezi na Katiba vilevile ni stakabadhi ya kiutekelezi. Katiba hueleza jinsi mambo yanafaa kufanywa na pia hutaja na kuelekeza kuhusu mambo tofauti. J.L Austin (1962) katika nadharia yake ya vitendo-usemi anasema kuwa usemi sio tu maneno kama watu wengi hufikiria lakini pia huashiria vitendo. Sheria hujikita sana katika utekelezi. Kwa mfano kwa kutoa maneno kama vile: ‘una hatia’ au ‘utalipa shilingi elfu kumi’ yana athari kwa yule anayelengwa. Nadharia ya *Skopos* ilitusaidia kuchunguza na kujadili endapo lengo la tafsiri linafikiwa au la. *Constitution of Kenya 2010* ni makala ya kisheria ambayo ilifaa kutafsiriwa kwa kulenga kudumisha maana za kiisimu pasina kupotosha maana za kisheria. Utafiti huu ulilenga kubaini kama lengo hili lilifikiwa au la.

Nadharia hii ilitufaa katika kufanya utafiti wetu katika kubaini mkinzano wa maana ulioko katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* hasa kwa kulenga kubainisha kama tafsiri hii imefikia viwango vya usawidi wa kisheria sawia na ilivyo katika matini chanzi. Nadharia hii inasisitiza nia ya tafsiri. Ili kutafsiri Katiba ya Kenya ni lazima kuelewa kwamba hii ni matini ya kisheria na ni lazima hili lidumishwe hata baada ya kufanya tafsiri. Mtafsiri asipokuwa na nia hii basi atatafsiri kwa maneno tu ya kawaida na mwishowe makala ile itaishia kupoteza urasmi wake na basi haitakuwa tena matini ya kisheria na atakuwa amefeli katika shughuli yake. Pia ni lazima kuwe na uwiano wa matini chanzi na matini lengwa. Katika utafiti wetu tulichunguza kama mshikamano huu wa matini upo au la. Katika utafiti huu pia tutatafsiri nyuma ili kubaini kama neno likitafsiriwa kutoka tafsiri ya Kiswahili hadi Kiingereza kama tutapata maana ile iliyokuwapo mwanzoni. Tulichunguza pia kama Katiba hii imefikisha ujumbe uliohitajika kwa msomaji bila kuupotosha.



### **1.9 Mbinu za Utafiti**

Tulikusanya data katika utafiti wetu hasa kutoka katika matini chanzi ambayo ni Katiba ya Kenya iliyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza (*Constitution of Kenya 2010*) na tafsiri yake ambayo imeandikwa kwa lugha ya Kiswahili (*Katiba ya Kenya 2010*). Data hii tuliitoa hasa katika Sura ya 3 inayohusu Uraia na Sura ya 4 ya *Katiba ya Kenya 2010* inayohusu Sheria ya Haki.

Baadaye tuliwasilisha data hii kwenye jedwali yenye safu mbili. Vifungu na maneno ya Kiingereza yatakuwa upande mmoja kisha yale ya Kiswahili upande mwingine lakini kila kifungu au kila neno lililingana na tafsiri yake. Tulichunguza kama maana ya kisheria iliyojitokeza katika matini chanzi ilidumishwa katika matini lengwa. Tulirejelea kamusi za kisheria kuelewa istilahi tofauti za kisheria zilizotumiwa katika uandishi wa Katiba na pia tukarejelea maktaba na mitandao katika uchunguzi zaidi. Kisha tulichukua data hiyo na kuichanganua kwa kutumia nadharia ya *Skopos* ambayo tulitumia katika utafiti wetu. Maswali na malengo ya utafiti yalitusaidia kuchanganua data hii na kisha kupata jibu la swali letu ambalo ni kuonyesha changamoto zinazojitokeza wakati wa kutafsiri matini ya kisheria ambayo ni *Constitution of Kenya 2010*.

## SURA YA PILI

### WASIFU WA SAJILI YA SHERIA NA CHANGAMOTO KATIKA KUTAFSIRI SHERIA

#### 2.0 Utangulizi

Sura hii itaangazia wasifu wa sajili ya sheria kwa kijumla kama hatua ya mwanzo ya kuwezesha kuiangalia Katiba kama matini ya kisheria. Sajili hii ina upekee sana na inahitaji mtafsiri awe na uelewa na udhibiti wa kutosha wa wasifu, taratibu na kaida zake licha ya kuwa mwangalifu hasa wakati wa kutafsiri. Kimsingi wasifu wa sajili ya kisheria unahusiana na mambo mengi yaliyo na mwelekeo wa kiufundi yanayojumuisha uwekezaji wa maana katika maneno, utumiaji wa istilahi zilizo na maana mahususi na utumiaji wa taratibu mahususi za kimaandishi. Mambo haya yamejadiliwa kwa sababu yamejitokeza katika Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Katiba ya Kenya 2010*.

#### 2.1 Wasifu wa Sajili ya Sheria

Matini za kisheria hutumia lugha kwa njia ya kipekee ambayo humhitaji mtafsiri azingatie sifa za lugha ya kisheria anapofanya utafiti wake ili kuzua tafsiri ambayo haina mikinzano yoyote ya kiisimu au kisheria. Mellinkoff (2003) anaeleza kuwa lugha ya kisheria huwa na sifa maalum. Kwanza lugha hii huwa na matumizi ya maneno ya kawaida ambayo yakitumika katika muktadha wa sheria huweza kuleta maaana ya kisheria. Kwa mfano neno '*serve*' kwa kawaida ina maana ya kumpa mtu kitu lakini katika lugha ya kisheria inamaanisha kuwasilisha makala ya kisheria kwa mtu fulani. '*To concur*' kwa kawaida inamaanisha kukubaliana na jambo fulani. Katika mazingira ya kisheria kama vile kortini hili linamaanisha kukubaliana na kile ambacho wakili mwingine amesema lakini kwa sababu tofauti kabisa. Maneno haya yakitumika katika muktadha wa kisheria itabidi mtafsiri awe makini katika kuyatafsiri ili kulenga maana iliyonuiwa kisheria na wala si ile ya kawaida.

Wasifu mmoja wa kimsingi kuhusiana na lugha ya sheria unahusu msamiati na mifanyiko ya kimsamiati kama vile matumizi ya maneno ya kawaida yanayoibua maana mahususi za kishere, matumizi ya vikale na msamiati wa mkopo. Maneno ya kale katika lugha ya Kiingereza ni kama vile; '*hereafter, hereof, thenceforth, therein na herewith*'. Tafsiri ya maneno haya ni kama vile;

**Hereafter** - baada ya hapa

**Thenceforth** - kuanzia hapo/hapa

**Hereof** - kuambatana na hili/hilo

**Therein** - humo ndani, mle ndani

**Herewith** - kuandamana na

Maneno haya hayawezi kutafutiwa maana yake katika kamusi moja kwa moja. Maana hii isipopatikana kulingana na kanuni ya tafsiri ni kwamba mtafsiri anaweza kutumia maelezo kuelezea dhana hizi. Hata hivyo, japo kanuni hii inaruhusu kutafsiriwa kimaelezo, kuna uwezekano wa kukinzana kwa kisawidi wa kisheria na kile cha kiisimu.

Wasifu mwingine na ambao una uwezekano wa kujitokeza katika Sura ya 3 na Sura ya 4 ni matumizi ya lugha ya kigeni. Vifungu na maneno mengi ya Kilatini huweza kutumika katika matini za kisheria kwa mfano, **ab initio**, **ex delicto** na **ex parte**. Maneno haya ni ya kigeni. Kanuni ya tafsiri ni kuwa kuna uwezekano wa maneno haya kupotea katika matini lengwa lakini maana iliyokusudiwa haipotei. Kwa mfano,

**ab initio** – tangu mwanzo

**Ex delicto** – kitu kinachotokana na dosari au kosa.

**Ex parte** – upande mmoja

Mfano kutoka lugha ya Kifaransa ni kama vile;

**force majeure** - nguvu nyingi sana.

Hivyo basi katika kutafsiri Katiba mtafsiri akitumia maelezo kuwakilisha maneno na vifungu vya kigeni kunatokea mkinzano wa ujitokezaji wa maana ya kiisimu ambayo haiakisi masharti na matarajio ya usawidi wa kisheria na matini ile inapoteza upekee wake kama matini ya kisheria.

Sifa nyingine ya sajili ya sheria ni kwamba lugha inayotumika huwa ya kiufundi na changamano na ambayo mara nyingi uhitaji uelewa wa masuala ya kisheria ili kuelewa maaana inayokusudiwa. Maneno haya ni kama vile,

*amicus curiae* – rafiki wa korti, rafiki wa mahakama

*lessee* – mpangaji

*felony* – kosa la uhalifu

Maneno haya yatahitaji kutafsiriwa kimaelezo kwa sababu hakuna istilahi ya moja kwa moja kutoka katika lugha ya Kiswahili inayoelezea maneno haya. Hili vilevile litazua changamoto katika tafsiri ile kwani kiwango cha usawidi wa kisheria hakitafikiwa.

Sifa nyingine ya sajili ya kisheria inahusiana na matumizi mengi ya maneno rasmi na mtindo unaotumika ni wa kitobinafsi ambao hauhusishwi na mtu maalum aidha mwanamke, mwanamme au kitu chochote. Hili huweza kuvuruga mawasiliano hasa mtu wa jinsia fulani anapoashiriwa au idadi fulani kujitokeza wazi lakini isitajwe. David Crystal na Derick Davy (1969) katika utafiti waliofanya kwa makala mia moja na nane walipata kuwa maneno ya Kiingereza kama vile ‘he, she, they, their, this, that’ na ‘it’ yalikosekana katika makala hayo ya kisheria. Baadhi ya maneno yanayotumika kuashiria wale wanaorejelewa katika sajili ya kisheria kama vile kortini ni **mshtakiwa, kiongozi wa mashtaka, jaji** na **shahidi**. Katika *Katiba ya Kenya 2010* katika Sura ya 3 na Sura ya 4 hakuna jinsia yoyote inayorejelewa aidha mke au mme. Katiba kwa mfano inarejelea wanaolengwa kama watu, raia au wananchi.

Sajiliya kisheria pia huwa na matumizi ya lugha yenye heshima na urasmi ili kuonyesha kuwa lugha hiyo ni tofauti na ile ya kawaida. Kwa mfano;

*approach the bench* badala ya *come here*

*prior* badala ya *before*

*subsequent* badala ya *after*.

Lugha hii huifanya stakabadhi yoyote ile kuwa rasmi na hivyo basi watu wanaichukulia kwa makini zaidi. Lugha hii pia huipa stakabadhi ile hadhi ya juu. *Constitution of Kenya 2010* imeandikwa kwa kutumia lugha rasmi na baadhi ya mambo yanayoonyesha urasmi huu ni kama vile matumizi ya maneno ambayo ni ya kitobinafsi bila kutaja jinsia yoyote.

Sajili ya kisheria pia huwa na maneno na vifungu vilivyo na maana isiyo wazi. Lugha huweza kuwa isiyoeleza kikamilifu jambo fulani. Baadhi ya maneno haya ni kama vile;

*Clear and convincing* – wazi na kusadikisha

*abuse of discretion* – ukiukaji wa hiari, matumizi mabaya ya hiari

*due process* – mchakato stahilifu

*improper* – sio sahihi

*extraordinary services* – huduma zisizo za kawaida

Richard C. Wydick (1998) na David Mellinkoff (1963) wanaeleza kuhusiana na sheria ambazo zinaweza kutumika kuandika makala ya kisheria ambayo yataeleweka kwa urahisi kwa kutumia lugha ya Kiingereza ya kawaida. Ingawaje Richard C. Wydick anaangazia kiwango cha sentensi Mellinkoff analenga makala ya kisheria kwa jumla. Richard C. Wydick anapendekeza kuwa inafaa watumie lugha inayoepuka maneno mengi na ya ziada, watumie vielezi, sentensi ziwe fupi, wapange maneno yao kwa uangalifu, watumie maneno ya kawaida na waakifishe kazi yao vizuri. David Mellinkoff naye anapendekeza lugha ya sheria iwe wazi, sahili, kabla ya kuandika na mtafsiri awe na makala ya kumwongoza katika tafsiri yake na asieleze jambo huku akirudia. Lugha sahili ya kisheria ikitumika itawezesha tafsiri mwafaka kufanywa na ujumbe kuwasilishwa bila tatizo au mtafaruku wowote.

Sajili ya sheria huwa na maneno ya kiutendaji ambayo yakitafsiriwa kwa Kiswahili huwa na utata. Maneno haya ni kama vile ‘**shall**’ na ‘**will**’. Matumizi ya maneno haya pia yatategemea yamesemwa na nani na katika muktadha gani. Yasipotafsiriwa vyema basi huenda kukaibuka utata wa maana. Katika *Constitution of Kenya 2010* maneno haya yametumika sana. Kwa mfano, Sura ya 4, Kifungu cha 43, ibara ya (3);

**Kielelezo 2;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
43 (3) The State <b>shall</b> provide appropriate <b>social security</b> to persons who are unable to support themselves and their <b>dependants</b> .	43 (3) Serikali itatoa <b>ulinzi wa kijamii</b> unaofaa kwa wale ambao hawezi kujisimamia wao wenyewe na <b>jamii zao</b> .

Tafsiri ya neno **shall** haipatikani moja kwa moja kutoka kwa kamusi yoyote. **Shall** hutumika kutilia mkazo lile ambalo linazungumziwa katika matini ya kisheria. Maelezo yametumika katika kutafsiri **shall** katika matini lengwa na matokeo yake ni kwamba maana iliyoibuka ni ya kiisimu na imekosa usawidi wa kisheria.

Sajili ya kisheria pia hutilia maanani uakifishaji. Kwa mfano;

- a) *a person who leaves two hundred dollars to each of my children who took care of me*
- b) *a person who leaves two hundred dollars to each of my children, who took care of me.*

Sentensi ya (a) ina maana ya mtu anayeacha dola mia mbili kwa watoto wake wote waliomsaidia ilhali sentensi ya (b) ina maana ya mtu ambaye huacha dola mia mbili kwa watoto mahususi ambao walimsaidia kumaanisha kuna wale ambao hawakumsaidia. Iwapo mtafsiri atakosa kuzingatia uakifishaji huu kunatokea ukinzani wa kimaana kati ya matini chanzi na matini lengwa.

Wasifu mwingine wa sajili ya kisheria ni kwamba katika sajili hii kuna uwepo wa matumizi ya maneno ambayo hayaleti maana kamili katika matumizi ya kawaida na yamekiuka sheria za kisarufi na hivyo kupata maana kamili lazima uwe na uelewa kuhusu maswala ya kisheria na lugha inayotumika kule. Kwa mfano; **‘of even date herewith’** badala ya **‘dated same as this document,’** **‘these presents’** badala ya **‘this document,’** **‘the date hereof’** badala ya **‘today,’** na **‘in my said mother’** badala ya **‘my mother.’** Maneno haya yatakuwa na maana tofauti hasa tafsiri isipofanywa kwa kutumia kiwango cha usawidi wa kisheria na maana huenda ikawa tofauti kabisa.

Sentensi katika sajili ya kisheria huwa ndefu sana na changamano. Mara nyingi huwa maswala mengi yanajadiliwa katika sentensi moja na hivyo kuyafanya yasieleweke kwa urahisi. Sentensi hizi zinaweza kugawanywa katika sehemu ndogo ndogo na maana kujitokeza vyema zaidi bila kubadili maana. Sentensi ndefu huwa vigumu sana kutafsiri. Lugha ya sheria pia huwa na urejeshi mwingi. Kwa mfano; **‘Player promises tha player will play...’** Mawakili hutumia sana nomino badala ya viwakilishi vyake na nomino hii hurudiwa sana.

Tafsiri za kisheria huwa na changamoto sana wakati wa kutafsiri na hivyo basi inahitaji ustadi wa juu ili kupata tafsiri iliyo bora zaidi. Tatizo kuu ni kupata istilahi mwafaka za kisheria bila kuwa na mkinzano wowote. Wataalam hawa ingawaje hawajaangalia tafsiri za kisheria ambazo zinahusiana na Katiba. Kutokana na mwanya huu utafiti wetu unachunguza tafsiri ya *Constitution of Kenya 2010* inapolinganishwa na matini chanzi ya Katiba ya Kiingereza (*Constitution of Kenya 2010*). Tunachunguza kwa kueleza kwa nini hali hii ikatokea. Utafiti tunaokusudia unaangazia kueleza mwafaka uliopo kati ya maana na sheria.

## **2.2 Wasifu wa Katiba kama Matini ya Kisheria**

*Constitution of Kenya 2010* imeandikwa kwa kufuata mtindo maalum ambao unaitambulisha kama matini ya kisheria na kuipa urasmi. Katiba hii imegawanywa katika sura kumi na nane. Kwa mfano sura tunazolenga katika utafiti wetu ni Sura ya 3 inayohusu Uraia na Sura ya 4 inayohusu Sheria ya Haki. Sura hizi zimegawika zaidi katika vifungu mbalimbali. Sura ya 3 kwa mfano ina Vifungu 7 kuanzia Kifungu 12-18. Vifungu hivi vinahusu haki za uraia, kupata na kudumisha uraia, uraia wa kuzaliwa, uraia wa kujiandikisha, uraia mara mbili, kupokonywa uraia na sheria kuhusu uraia. Vifungu hivi navyo vimegawika zaidi katika ibara. Kwa mfano Sura ya 3, Kifungu cha 13 kuna ibara tatu ambazo ni;

**Kielelezo 3;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<p>13. Retention and acquisition of citizenship</p> <p>(1) Every person who was a citizen immediately before the effective date retains the same citizenship status as of that date.</p> <p>(2) Citizenship may be acquired by birth or registration.</p> <p>(3) Citizenship is not lost through marriage or the dissolution of marriage</p>	<p>13. Kupata na kudumisha uraia</p> <p>1) Kila mtu ambaye alikuwa raia punde tu kabla ya kuanza kutumika Katiba hii atadumisha hali ya uraia wake.</p> <p>2) Uraia unaweza kupatikana kwa kuzaliwa au kujiandikisha.</p> <p>3) Uraia haupotezwi kwa sababu ya ndoa au kuvunjika kwa ndoa.</p>

Katiba ina matumizi ya istilahi maalum za kisheria. Istilahi hizi huwa zinatokana na lugha za kigeni na mara nyingi katika katiba huwa zimenukuliwa jinsi zilivyo bila kutafsiriwa kwa neno mbadala au kutafsiriwa kwa kutumia maelezo. Kwa mfano;

**Kielelezo 4;**

Sura ya 4 Kifungu cha 51, ibara ya (2);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<p>(2) A person who is detained or held in custody is entitled to petition for an order of <i>habeas corpus</i>.</p>	<p>(2) Mtu yeyote aliye kizuizini ama aliyezuiliwa ana haki ya kulalamika ili kutolewa amri ya <b>kufikishwa mahakamani</b>.</p>

**Kielelezo 5;**

Sura ya 4, Kifungu cha 58, ibara ya (6) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<p>(6) (b) shall not take effect until it is published in the <i>Gazette</i>.</p>	<p>(6) (b) Haitatekelezwa hadi ichapishwe kwenye Gazeti rasmi la serikali.</p>

**Kielelezo 6;**

Sura ya 8, Kifungu cha 97, ibara ya (1) (d);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<p>(1) (d) the Speaker, who is an <i>ex officio</i> member.</p>	<p>(1) (d) Spika, ambaye ni mwanachama <i>m'badala</i>.</p>



Katika mifano hii ni kwamba maneno haya; *habeas corpus*, *Gazette* na *ex officio* yameendelezwa moja kwa moja yalivyo katika lugha ya kigeni bila kutafsiri kwa Kiingereza. Hili hukubaliwa iwapo tafsiri mwafaka haipatikani katika lugha lengwa. Tatizo linalojitokeza ni kuwa wakati wa kutekeleza sheria hii inaweza ikawa vigumu kwa wananchi kuelewa maana ya maneno haya kwa kurejelea muktadha.

Katiba ina matumizi ya sentensi ndefu na changamano. Changamoto katika kutafsiri Katiba kutoka matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*) hadi matini lengwa (*Katiba ya Kenya 2010*) zimejitokeza sana hasa kutokana na urefu wa sentensi hizi. Sentensi au kauli fupi huwa rahisi kutafsiri ikilinganishwa na ndefu ambazo huwa na hoja nyingi ambazo kutafsiri itakuwa vigumu. Kwa mfano katika Sura ya 4 Kifungu cha 27 ibara ya 6;

**Kielelezo 7;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(6) To give full <b>effect</b> to the realization of the rights guaranteed under this Article, the state Shall take legislative and other measures, including affirmative action programmes and policies <b>designed to redress any disadvantage suffered</b> by individuals or groups because of past discrimination.	(6) Ili kutoa <b>athari</b> kamilifu za kutimiza haki zinazohakikishiwa na Kifungu hiki, Serikali itachukua hatua za kisheria na nyinginezo kukiwemo vitendo sawazishi na sera ambazo <b>zimebuniwa kupinga athari za kutonufaika</b> kwa watu binafsi au makundi ya watu kwa sababu ya ubaguzi wa hapo awali.

Katika kutafsiri sentensi hii inakuwa vigumu kwa mtafsiri kuhawilisha mawazo yaliyo katika MC hadi ML kwa njia mwafaka. Kwa mfano tafsiri ya *designed to redress any disadvantage suffered* ni ‘*zimebuniwa kupinga athari za kutonufaika*’. Tafsiri hii haijazingatia tafsiri yaliyomo. Kwa mfano; *redress* si kupinga bali ni kufidia au kurekebisha, hivyo hivyo *disadvantage* ni kasoro, hitilafu, mapungufu fulani ilhali *suffered* inaweza kuwa –liteseka, -libaguliwa au –litengwa. Tafsiri hii ingekuwa ‘zimebuniwa kufidia hitilafu zozote za kutonufaika’. Hili linazua tafsiri potovu.

Katiba kama makala ya sheria ina matumizi ya maneno kama vile ‘**shall**’ na ‘**will**’ ambayo katika kutafsiri pia huwa ni vigumu. Kwa mfano katika Sura ya 4 Kifungu cha 30;

**Kielelezo 8;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
30. Slavery, servitude and forced labour (1) A person shall not be held in slavery or servitude. (2) A person shall not be required to perform forced labour.	30. Utumwa na kazi ya kulazimishwa (1) Hakuna mtu atazuiliwa katika utumwa. (2) Mtu hatahitajika kufanya kazi ya kulazimishwa

Matumizi ya ‘shall’ na ‘will’ hutumika hasa kuisisitiza utekelezaji wa jambo na sharti jambo lile litekelezwe. Katika uandishi wa kisheria neno ‘shall’ huashiria ulazima, uwajibikaji au ushurutikaji zaidi kuliko ‘will’ ambao huelekea kuonyesha uwepo wa uwezekano mbadala. Katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* hasa kwa kuangazia Sura ya 3 na Sura ya 4, maneno haya yametafsiriwa kwa njia zinazotofautiana hivi kwamba msisitizo uliokuwepo katika lugha ya Kiingereza haupatikani katika tafsiri ya Kiswahili. Tafsiri yake ni kwamba ‘...hakuna...’ ambayo ina maana ya ‘...there is no...’ Hapa maana iliyokusudiwa imevurugika na tafsiri kupoteza urasmi wa matini ya kisheria.

Katiba pia ina urejelezi wa vifungu katika maelezo yake. Kwa mfano katika Sura ya 3, Kifungu cha 12, ibara ya (2);

**Kielelezo 9;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) A passport or any other document referred to in clause (1) (b) may be denied, suspended or confiscated only in accordance with an Act of Parliament that satisfies the criteria referred to in Article 24.	(2) Hati ya usafiri au hati nyingine ya usajili au utambulisho iliyotajwa katika ibara ya (1) (b), inaweza kunyimwa mtu, kusimamishwa kwa muda au kupokonywa mtu kwa mujibu wa Sheria ya Bunge ambayo inatosheleza kigezo kilichotajwa katika Kifungu cha 24.

**Kielelezo 10;**

Katika Sura ya 3, Kifungu cha 14, ibara ya 2,

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) Clause (1) applies equally to a person born before the effective date, whether or not the person was born in Kenya, if either the mother or father of the person is or was a citizen.	(2) Ibara ya (1) itatumika sawa kama mtu ambaye alizaliwa kabla ya siku ya kuanza kutumika kwa Katiba hii, iwe amezaliwa nchini au la, ikiwa mama au baba yake ni, au alikuwa raia.

Mifano hii inahitaji msomaji kurejelea aliyosoma katika vifungu na ibara zilizotangulia ili kujua masharti au maelezo yanayotolewa. Mfano wa kwanza msomaji itahitaji arejelee hati ya utambulisho inayotajwa katika ibara ya (1) (b) ambayo ni hati ya usafiri ya Kenya au hati yoyote ya usajiliwa inayotolewa na Serikali kwa raia wake. Mfano wa pili nao unarejelea ibara ya (1) ambayo inaeleza kuhusu kupata uraia nchini Kenya iwapo wazazi wote ni raia iwe umezaliwa nchini au la. Ibara ya (2) inatoa maagizo kuhusu wakati ambapo sheria hii itanza kutumika.

Sifa moja inayojitokeza katika uandishi wa Katiba kama matini ya kisheria ni urudiaji wa maneno kwa njia ya kuweka msisitizo. Mara nyingi hili hufanyika ili kuweka wazi kile ambacho kinazungumziwa bila kuleta utata wowote katika kufasiri kwake wakati wa utekelezaji. Kwa mfano katika Sura ya 11, Kifungu cha 182, ibara ya (2);

**Kielelezo 11;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) If a vacancy occurs in the office of the county governor, the deputy county governor shall assume office as county governor for the remainder of the term of the county governor.	(2) Iwapo ofisi ya gavana wa kauti itakuwa wazi, naibu gavana atatekeleza majukumu ya gavana kwa kipindi kilichosalia cha gavana kuhudumu.

*County governor* imerudiwa ili kuonyesha bayana yule anayestahili kuchukua wadhifa wa gavana iwapo nafasi hii itawachwa wazi. Urudiaji huu unaojitokeza una uamili mahususi, kuweka jambo bayana kadri iwezekanavyo. Urudiaji huu umeondoa utata wowote kwa kueleza wazi yule anayerejelewa ama ni naibu gavana wa kaunti au gavana wa kaunti mwenyewe.

Katiba pia ina matumizi ya maneno ya kawaida ambayo yana maana tofauti kisheria. Sura ya 17, Kifungu cha 260 katika *Constitution of Kenya 2010* kuna maelezo kuhusu maneno yaliyotumika na tafsiri yake. Kwa mfano;

**Kielelezo 12;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
“disability” includes any physical, sensory, mental, psychological or other impairment, condition or illness that has, or is perceived by significant sectors of the community to have, a substantial or long-term effect on an individual’s ability to carry out ordinary day-to-day activities;	‘ulemavu’ inamaanisha ulemavu wowote wa kimwili, kihisia, kiakili, kisaikolojia au ulemavu wa aina nyingine, hali au ugonjwa ambao, au unaochukuliwa na sekta mahususi za kijamii kuwa na athari za muda mrefu kwa mtu kuweza kutekeleza majukumu yake ya kawaida ya kila siku;

Maelezo haya hutumika ili kuelezea istilahi ambazo zinaweza kuwa tata na kuweka bayana maelezo yake. Ulemavu huchukuliwa kwa kawaida kama mtu aliyelemaa mwili peke yake. Maelezo haya ya Katiba yametoa maana zaidi ya neno hili kama mtu yeyote mwenye ulemavu wa kihisia, kiakili au kisaikolojia.

**2.3 Usawidi wa Kisheria**

Usawidi wa kisheria unahusu kuandika kwa njia zinazoakisi masharti, matarajio, maelezo, maelekezi na utoshelevu wa kisheria kwa jumla. Matini za kisheria huwa na matumizi ya lugha ya kipekee katika muktadha wa sheria na ambayo huhitaji umakinifu hasa katika kuzingatia sifa za sajili ya kisheria ili kuweza kuitambulisha. Lugha ya kisheria huwa ni tofauti sana na ile inayotumika katika hali ya kawaida. Matini za kisheria hutumia lugha iliyowekezwa sifa na maana za kisheria ili kuonyesha upekee wake kama lugha ya kisheria. Mtafsiri ni lazima atilie maanani kuwa istilahi za kisheria hutegemea muktadha ambapo zimetumika na maana inaweza kubadilika kutegemea pale zilipotumika. Hii ndiyo sababu matumizi ya kamusi hayafai katika kufanya tafsiri za matini za kisheria kwa kuwa maana za maneno hubadilika kutegemea muktadha. Tafsiri mwafaka inahitaji uelewa wa mada inayojadiliwa na mtafsiri anaweza kutumia matini zingine ambazo zimetafsiriwa na ambazo zimeangazia mada ile ili kuelewa kikamilifu jinsi ya kufanya tafsiri yake.

Matini za kisheria huwa na matumizi ya lugha ya kipekee ambayo huhitaji mtafsiri kuwa makini katika kuitafsiri ili kuhakikisha kuwa upekee ule umedumishwa katika ML. Istilahi zinazotumika katika matini za kisheria huweza kubadilika kutegemea muktadha na hii ndiyo sababu kamusi huwa hazitumiki sana. Lugha katika matini za kisheria pia

huweza kufuata mtindo mahususi wa uandishi na ambao si rahisi kubadilika kwa sababu unafuata fomula maalum ya uandishi wa makala ya kisheria. Hii ina maana kuwa matini za kisheria lazima zifuate mkondo maalum na ili kufanya hivi lazima lugha iwe isiyobadilika kwa urahisi ili kudumisha mtindo ule. Hivyo basi uteuzi na matumizi ya maneno katika matini ya kisheria si kwa kubahatisha tu na iwapo mabadiliko yoyote yatafanywa basi kutatokea athari za kisheria.

Matini za kisheria uhitaji pia mtafsiri azingatie kwa makini kila neno au hata uakifishaji wowote uliofanywa katika MC. Hili linapotekelezwa matini za kisheria huonekana kuwa zenye maneno mengi na urudiaji unajitokeza sana. Kwa mfano katika *Constitution of Kenya 2010* kuna urudiaji ambao umejitokeza sana na mtafsiri ameshawishika kubadilisha vifungu hivi na kuondoa uradidi huu. Matini hizi pia huwa na matumizi ya sentensi ndefu na changamano ambazo huzua changamoto kwa mtafsiri wakati wa kufanya tafsiri. Maneno ya kigeni kama vile ya Kilatini na Kifaransa pia hutumika katika matini za kisheria. Ili mtafsiri awe na makala athirifu lazima azingatie haya ili kudumisha usawidi wa kisheria.

*Constitution of Kenya 2010* ni matini ya kisheria ambayo inahitaji kutafsiriwa kwa kulenga kuafiki usawidi wa kisheria. Katika kufanya tafsiri hivi, ni muhimu mtafsiri amakinike kwa kuzingatia kila neno kwa sababu kosa moja linaweza kuzua maana tofauti sana na iliyonuiwa. Tafsiri ya *Constitution of Kenya 2010* katika lugha ya Kiswahili imezingatia kiwango cha kiisimu peke yake ambayo imefanya matini ile kukosa kufikia lengo lake la kuonekana kamamatini ya kisheria. Matini hii haiwasilishi maana ya kisheria au hata kuhawilisha maana iliyoko katika matini chanzi. Ingawaje hatuwezi kupuuza masuala ya kiisimu kikamilifu, kuna umuhimu wa mtafsiri kutilia maanani kuwa anatafsiri matini ya kisheria na hivyo basi kuzingatia na kuafiki masharti na matarajio ya usawidi wa kisheria. Tathmini ya Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010* inaonyesha kuwa tafsiri hii ilifanywa kwa njia potovu pasina kuzingatia masharti yanayohusiana na usawidi wa kisheria. Maana ambazo zimekezwa katika kila neno kisheria hazikuzingatiwa kikamilifu na hili lilizua mkinzano na kimaana kati ya matini chanzi na matini lengwa.

Katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* mambo yafuatayo yanafaa kutiliwa maanani ilikuzua tafsiri mwafaka;

- (a) Mtafsiri anafaa kuwa anaelewa kikamilifu masharti na taratibu za kiuandishi kuhusiana na taaluma ya kisheria na mada inayolengwa katika hali hii *Katiba ya Kenya 2010*.
- (b) Mtafsiri anafaa kuwahusisha wataalam wanaoelewa zaidi mada inayolengwa ili kuelewa kilichokusudiwa wakati matini ile ikiandikwa.
- (c) Mtafsiri anafaa kuhakikisha kuwa kila kitu ambacho kilihitaji kutafsiriwa katika matini chanzi kimetafsiriwa na kwamba hakuna neno lolote limeachwa, uakifishaji umezingatiwa na wala hakuna sentensi, kifungu au ukurasa ulioachwa bila kutafsiriwa. Kutafsiri Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010* kumekumbwa na matatizo haya.
- (d) Mtafsiri anafaa kuzingatia tarakimu na tarehe katika matini chanzi bila kuzibadilisha kuwa maneno.

Matini za kisheria hivyo basi ni lazima zizingatie wasifu wa lugha ya kisheria na lugha ile lazima iwe isiyobadilika kwa urahisi kwani inafuata mtindo maalum wa kisheria. Hii ina maana kuwa lugha ya kisheria huwa inafuata mkondo fulani wa kitamaduni na ambao lazima uendelezwe katika tafsiri. Matumizi ya maneno au vifungu vya maneno katika matini za kisheria si kwa kibahati tu. Kuna sababu ya kila neno au kifungu kutumika katika muktadha fulani na iwapo kutakuwa na mageuzi, basi kutatokea athari za kisheria. Mtafsiri anafaa pia kuzingatia istilahi za kisheria ambazo zinakaribiana kimaana lakini zina maana tofauti. Kwa mfano katika *Constitution of Kenya 2010*, kuna tofauti kati ya ***right*** na ***entitlement***. Maneno hayani vigumu sana kuonyesha tofauti iliyopo katika lugha ya Kiswahili. Katika kutafsiri lugha ya kisheria tofauti zile ni muhimu kuonyeshwa katika matini lengwa. Iwapo maneno yamerudiwa pia ni muhimu mtafsiri ahakikishe kuwa anayatafsiri kwa kuyarudia jinsi yalivyo na hafai kamwe kuyabadilisha. Katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* kuna sehemu ambapo mtafsiri anabadilisha maneno yaliyorudiwa.

## 2.4 Changamoto katika Kutafsiri kwa Kuegemea Usawidi wa Kisheria

Moja ya changamoto ya kimsingi katika kutafsiri sheria inahusiana na hujitokeza hasa kutokana na istilahi za kisheria zinazotumika. Kinyume na taaluma nyingine kama vile za kisayansi ambazo istilahi zake ni bia, istilahi za kisheria huwa ni tofauti kutegemea nchi husika na tamaduni husika. Ili kupata tafsiri mwafaka inahitaji mtafsiri awe na uelewa wa hali ya juu wa istilahi za kisheria na mfumo mzima wa kisheria wa nchi husika. Kutafsiri sheria kunahitaji umakinifu na tafsiri sahihi lazima ifanywe. Katika *Constitution of Kenya 2010* kuna matumizi ya istilahi ambazo kupata tafsiri mwafaka katika lugha ya Kiswahili inakuwa na utata. Kwa mfano katika Sura ya 3, Kifungu cha 15, ibara ya (2);

### Kielelezo 13;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) A person who has been lawfully resident in Kenya for a continuous period of at least seven years, and who <b>satisfies the conditions prescribed by an Act of Parliament</b> , may apply to be registered as a citizen.	(2) Mtu ambaye amekuwa mkazi halali nchini Kenya kwa muda wa miaka saba mfululizo, na ambaye <b>anatimiza masharti yote yasheria yalioidhinishwa na Bunge</b> , na anaweza kutumia maombi ya kujiandikisha kama raia.

Katika Kifungu hiki, *satisfies the conditions prescribed by an Act of Parliament*, imetafsiriwa kama *anatimiza masharti yote ya sheria yalioidhinishwa na Bunge*. Tafsiri hii inaonekana kuwa na ugiligili. Kulingana na maoni yetu tafsiri hii inafaa kuwa *anakidhi masharti yote yaliyoagizwa na Sheria ya Bunge*.

Matumizi ya maneno kama vile ‘**shall**’ na ‘**will**’ yamezua changamoto katika kutafsiri. Maneno haya huwa hasa yanatilia mkazo na kuonyesha kwamba lazima mambo fulani yatekelezwe. Katika kutafsiri kwake basi maneno haya katika Katiba huwa vigumu sana kuyatafsiri. Kwa mfano;

### Kielelezo 14;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(55) The state <b>shall</b> take measures, including affirmative action programmes, to ensure that youth-	(55) Serikali <b>itachukua</b> hatua, miradi ya vitendo sawazishi, kuhakikisha kwamba vijana-
(57) The state <b>shall</b> take measures to ensure the rights of older persons-	(57) Serikali <b>itachukua</b> hatua kuhakikisha kuwa haki ya wazee-

Katika kutafsiri *shall* kwa Kiswahili inakuwa na changamoto sana kwani neno hili linafaa kuisisitiza yale ambayo yatatekelezwa lakini haya hayajitokezi wakati tafsiri ya Kiswahili inapofanywa. Tafsiri hii imefanywa kwa kutumia maelezo kueleza yatakayofanyika. Haya yanapofanyika basi Katiba ile inapoteza urasmi na kuacha kuonekana kama stakabadhi ya kisheria bali stakabadhi inayoeleza mambo kwa kijumla tu bila kuzingatia kigezo cha kisheria.

Katiba kama stakabadhi ya kisheria ina matumizi ya sentensi ndefu na ambazo ni changamano. Sentensi hizi ndefu huleta utata katika kutafsiri hasa katika kuhakikisha kuwa mawazo yote yaliyo katika matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*) yamehawilishwa ilivyo hadi katika matini lengwa (*Katiba ya Kenya 2010*). Kwa mfano katika Sura ya 13, Kifungu cha 221, ibara ya (6);

**Kielelezo 15;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(6) When the estimates of national government expenditure, and the estimates of expenditure for the Judiciary and <b>Parliament</b> have been approved by the <b>National Assembly</b> , they shall be included in an Appropriation Bill, which shall be introduced into the <b>National Assembly</b> to authorize the withdrawal from the Consolidation Fund of the money needed for the expenditure, and for the appropriation of that money for the purposes mentioned in the Bill.	(6) Wakati makadirio ya matumizi ya serikali ya kitaifa, makadirio ya matumizi ya mahakama na <b>Baraza la Kitaifa</b> , yatakuwa yameidhinishwa na <b>Baraza la Kitaifa</b> , yatajumlishwa katika Mswada wa Matumizi ya Fedha, utakaowasilishwa kwa <b>Baraza la Kitaifa</b> ili kuidhinisha kutolewa kwa fedha za matumizi kutoka kwa Mfuko wa Jumla, na matumizi ya fedha hizo kwa madhumuni yaliyotajwa katika mswada.

Kutafsiri kwa kifungu kumekumbwa na changamoto kama vile ukosefu wa istilahi mwafaka za kutumika. *Consolidation Fund* inatafsiriwa kama *Mfuko wa Jumla*. Tafsiri hii ina utata kwa sababu tukitafsiri kwa Kiingereza tena hatutapata maana ile ile iliyopo katika matini chanzi. Hili litampa msomaji maana potovu ambayo haipatikani katika matini chanzi.

Katiba pia ina matumizi ya maneno ya kawaida ambayo katika sheria yana maana tofauti. Katika Sura ya 17, Kifungu cha 260, Katiba imetoa maelekezo kuhusu maneno tofauti ambayo yametumika katika Katiba na ambayo kisheria yana maana tofauti na ile ya kawaida. Hili litazua utata katika kutafsiri iwapo mtafsiri atazingatia maana tu za kiisimu bila kutilia maanani maana za kisheria na hili likitokea basi ujumbe uliokusudiwa



kupitishwa kwa hadhira hautawafikia kwa njia inayostahili. Kwa mfano katika Sura ya 3, Kifungu cha 12, ibara ya (1);

**Kielelezo 16;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
1) Every citizen is entitled to: a) The <b>rights, privileges and benefits</b> of citizenship, subject to the limits provided or permitted by this constitution	1) Kila raia; a) Anastahili kupata <b>haki, fursa na faida</b> kwa mujibu wa katiba hii

Katika ibara hii, neno *benefits* limetafsiriwa kama *faida*. Katika matumizi ya kawaida hasa katika ulingo wa biashara neno hili linamaanisha mapato ya ziada ambayo mtu hupata baada ya kufanya biashara lakini katika sheria haliwezi likatafsiriwa kumaanisha *faida*. Tukitafsiri nyuma itakuwa *profit* na wala si *benefits*. Neno hili labda lingetafsiriwa kama *mafao*.

Matatizo pia yanajitokeza hasa kutokana na maneno ambayo yamekopwa kutoka lugha zingine. Maneno haya huwa vigumu kutafsiri nahasa kupata neno mwafaka linaloweza kuwasilisha ujumbe uliokusudiwa. Kwa mfano katika Sura ya 7, Kifungu cha 89, ibara ya 12;

**Kielelezo 17;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(12) For the purpose of this Article, ‘ <b>population quota</b> ’ means the number obtained obtained by dividing the number of inhabitants of Kenya by the number of constituencies or wards, as applicable, into which Kenya is divided under this Article.	(12) Kwa sababu ya Kifungu hiki, ‘ <b>idadi ya watu</b> ’ ina maana ya idadi inayopatikana baada ya kugawa idadi ya watu wanaoishi Kenya kwa idadi ya maeneo bunge au wadi, ifaavyo, kwa namna ambayo, Kenya ilivyogawanywa chini ya Kifungu hiki.

Tafsiri hii ni potovu pale ambapo *population quota* imetafsiriwa kama *idadi ya watu*. *Idadi ya watu* inamaanisha *population* na wala si *population quota*. Istilahi hizi katika uandishi wa Katiba zimenukuliwa moja kwa moja bila kutafuta maneno mbadala kwa lugha ya Kiingereza. Maneno haya baadaye yanakuwa na changamoto kwa mtafsiri kuyatafsiri kwa lugha zingine. Katika tafsiri ya Kiswahili maneno haya hayajaendelezwa kama yalivyo katika Katiba ya Kiingereza na kutafsiriwa kwake kumekumbwa na

changamoto. Tafsiri hii kwa maoni yetu ingekuwa ‘kiasi au mgao mahususi wa idadi ya watu’ kwa sababu *population quota* si umati wowote wa watu lazima uwekewe mipaka. Kwa mfano;

**Kielelezo 18;**

Sura ya 4, Kifungu cha 51, ibara ya (2);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) A person who is detained or held in custody is entitled to petition for an order of <b>habeas corpus</b> .	(2) Mtu yeyote aliye kizuizini ama aliyezuiliwa ana haki ya kulalamika ili kutolewa <b>amri ya kufikishwa mahakamani</b> .

**Kielelezo 19;**

Sura ya 4, Kifungu cha 58, ibara ya (6) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(6) (b) shall not take effect until it is published in the <b>Gazette</b> .	(6) (b) Haitatekelezwa hadi ichapishwe kwenye <b>Gazeti rasmi la Serikali</b> .

**Kielelezo 20;**

Sura ya nane, Kifungu cha 97, ibara ya (1) (d);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(1) (d) the Speaker, who is an <b>ex officio member</b> .	(1) (d) Spika, ambaye ni <b>mwanachama m’badala</b> .

Changamoto zimejitokeza katika kutafsiri maneno kama vile *haebas corpus* imetafsiriwa na maana yake kupotoshwa ambapo mtafsiri ametafsiri kama *amri ya kufikishwa mahakamani*, ambayo kwa hakika maana yake ni kushtakiwa na ilhali maana linganifu ni amri ya kuwasilishwa mahakamani. Maneno haya *habeas corpus* yamebebehsa fahiwa ya kisheria au kanuni ya kisheria ambayo inashurutisha kuwasilishwa kwa kuzingatia kanuni za usawidi wa kisheria ambapo mojawapo ya wasifu wa sajili ya kisheria ni matumizi ya maneno ya kigeni. Katika Sura ya 4, Kifungu cha 58, ibara ya (6) (b) *Gazette* imetafsiriwa kama *Gazeti rasmi la Serikali*. Katika Sura ya 8, Kifungu cha 97, ibara ya (1) (d) vilevile *ex officio* imetafsiriwa kama *mwanachama mbadala*. Athari za tafsiri hizi ni kwamba zimelenga maana za kiisimu na kwamba hazizingatii fahiwa za kisheria zilizokusudiwa kuwasilisha katika tafsiri. Kwa mfano, *ex officio* ni kanuni ya kisheria yenye maana *kwa misingi ya wadhifa wake*.

Urudiaji katika matini ya kisheria hukusudia kuhakikisha usahihi na uwazi wa kile kinachosemwa. Katiba ina matumizi ya maneno ambayo yanarudiwarudiwa. Urudiaji huu unazua changamoto katika kutafsiri kwani wakati mwingine mtafsiri huweza kukosa kuuzingatia na hivyo kuzua tafsiri potovu. Kwa mfano katika Sura ya 8, Kifungu cha 114, ibara ya (3);

**Kielelezo 20;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
3) In this constitution, “a money Bill” means a Bill, other than a Bill specified in Article 218, that contains provisions dealing with-	3) Katika Katiba hii, ‘Mswada wa Fedha’ unamaanisha, Mswada, tofauti na Mswada uliotajwa katika Kifungu cha 218 kilicho na masharti yaliyoshughulikia-

Katika Kifungu hiki neno *money bill* limetumika mara kadhaa katika Sura hii lakini katika kila Kifungu neno hili lina maana tofauti. Utata utakaojitokeza ni kwamba huenda mtafsiri asipate maneno mwafaka kutofautisha maneno yale katika kila Kifungu. Pia katika kutafsiri MC mtafsiri ameongezea koma baada ya neno ‘unamaanisha’ ambalo halikuwepo katika MC. Hii ni kinyume na kanuni za kutafsiri matini za kisheria ambapo mtafsiri anafaa kutafsiri MC bila kubadili chochote ndipo asibadili maana

**2.5 Jinsi ya Kukabiliana na Changamoto Zinazojitokeza katika Kutafsiri Sheria**

Tafsiri za matini za sheria zinahitaji kuwa ujumbe uliomo katika matini chanzi udumishwe katika matini lengwa na kwamba tafsiri ifanywe kwa ufasaha na kuhakikisha kuwa ujumbe huu haupotoshwi kwa vyovyote vile. Wakati ambapo mtafsiri amekosa neno mbadala wakati wa kutafsiri katika jamii lengwa anaweza kuacha istilahi hiyo jinsi ilivyo katika lugha ya kigeni ili kuhakikisha kuwa maana haijapotoshwa na imebaki ilivyo bila kupoteza ujumbe. Hili litajitokeza pale ambapo mtafsiri anatafuta neno mbadala katika lugha lengwa bila mafanikio. Istilahi hizi zikibaki bila kubadilishwa ingawaje huweza kuleta utata katika kutekelezwa kwake kwani mawakili na wengine watakozitumia huenda wakakosa kuzielewa na hivyo kuwa na wakati mgumu kuzielewa. Tafsiri ya neno kwa neno inaweza kuleta maana tofauti ambayo haihusiani na makala hayo na hata kuupotosha ujumbe zaidi. Hii ndiyo maana watafsiri wengi watatumia njia mbadala ya kutafsiri ili kuhakikisha kuwa hakuna neno moja limeachwa

bila kutafsiriwa. Hili linazuia utata unaoweza kujitokeza baadaye na hivyo wanaamua kutafsiri kila kitu ili kutoa tafsiri iliyo mwafaka.

Tafsiri za kisheria zimefungwa na sheria na ni lazima kuhakikisha kuwa katika kutafsiri makala yoyote mtafsiri lazima awe na ujuzi wa hali ya juu. Mtafsiri mzuri wa sheria lazima awe na uelewa wa maswala ya kiisimu, maswala ya kisheria na pia awe na ile hamu ya kutafsiri huku akifanya tafiti kila mara kuhusu mifumo tofauti ya kisheria. Mtafsiri lazima kwanza aelewe matini chanzi na ujumbe uliomo ndiposa aweze kutoa tafsiri mwafaka ya matini lengwa. Inafaa pia aelewe lengo la tafsiri yake ni gani kwa sababu hili litaathiri jinsi atakavyofanya tafsiri yake. Kwa mfano istilahi zilizotumika, miundo ya sentensi na toni inayotumika zinafaa kuzingatiwa ili kupata tafsiri mwafaka

Hivyo basi mtafsiri lazima awe na umilisi wa lugha zote za matini chanzi na matini lengwa, aelewe istilahi zinazotumika na mwishowe aelewe mfumo mzima wa sheria katika jamii anamofanya tafsiri. Tafsiri ya neno kwa neno hasa katika kutafsiri makala ya kisheria huzua tafsiri potovu. Miundo ya sentensi huwa ni tofauti kutegemea lugha inayotumika. Kwa mfano miundo ya sentensi katika lugha ya Kiswahili ni tofauti na ile iliyo katika lugha ya Kiingereza au Kifaransa. Hivyo basi mtafsiri atahitaji kuelewa lugha zinazotumika vizuri ili kufanya tafsiri mwafaka.

## **2.6 Hitimisho**

Tafsiri za kisheria zinahitaji mtafsiri kutumia lugha huku akitilia maanani maswala ya sheria na si ya kiisimu peke yake. Sheria hutegemea tamaduni husika na hivyo basi kutafsiri matini yoyote ya kisheria si rahisi na kuna changamoto nyingi sana hasa kama mtafsiri haelewi mfumo wa sheria wa jamii husika. Changamoto hizi zinaweza kupunguzwa ikiwa mtafsiri atakuwa mwangalifu akijua kwamba nia kuu ni kupitisha ujumbe kwa hadhira lengwa bila kuupotosha. Iwapo atakosa kuwa mwangalifu basi kutatokea utata katika kutekeleza sheria ile.

## **SURA YA TATU**

### **TATHMINI YA SURA YA 3 YA *CONSTITUTION OF KENYA 2010***

#### **3.0 Utangulizi**

Katika sura hii tulichanganua kwa kina Sura ya 3 na kuonyesha kuwepo kwa changamoto za kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* zinazohusiana na ujitokezaji wa mikinzano ya kimaana katika misingi ya kiisimu na misingi ya kisheria. Tulionyesha hivi kwa kuchukua data kutoka kwenye matini chanzi (*Constitution of Kenya 2010*) na kuiwasilisha katika jedwali huku tukiilinganisha kwa upande mwingine na ile ya matini lengwa (*Katiba ya Kenya 2010*). Kila kifungu kililingana na tafsiri yake na pia tukakoleza wino vifungu vinavyokinzana kimaana. Tulifanya mijadala kuhusiana na pale ambapo tulikisia kulikuwa na makosa, utohakika au makosa ya tafsiri.

#### **3.1 Ufafanuzi wa Sura ya 3**

Sura ya 3 inahusu Uraia na inaeleza kwa kina haki za kila raia nchini Kenya. Kila raia anapata uraia wakekwa kuzaliwa au kwa kujiandikisha. Mtu ambaye ni raia kwa kuzaliwa hapotezi uraia huu kwa kupata uraia wa nchi nyingine; ana haki ya uraia mara mbili. Mtu atapokonywa uraia wake iwapo alijisajili kwa njia ya ulaghai kuwa raia, alifanya biashara na adui au ikiwa amepatikana na hatia ya uhaini. Adhabu anayoweza kupewa ni kama adhabu ya kifungo cha miaka saba au zaidi au hukumu zaidi inaweza kutolewa. Bunge limepewa uwezo wa kutunga sheria zinazohusu uraia na kuhakikisha kuwa masharti yaliyotolewa kuhusu uraia yamefuatiliwa. Malengo ya sura hii ni kuhakikisha kuwa Serikali inajua idadi sawa ya wananchi wake wote na inaweza kubaini wageni wowote ambao watawasili nchini bila stakabadhi yoyote na kutishia usalama wa wananchi bila kibali.

#### **3.2 Ukinzani wa Maana Unaojitokeza katika Kutafsiri Sura ya 3 ya *Constitution of Kenya 2010***

Wasifu mmoja unaojitokeza katika *Katiba ya Kenya 2010* kama matini tafsiri ni ujitokezaji wa ukinzani wa kimaana ambapo dhana moja mahususi inatafsiriwa kwa njia mbadala na ilhali maana yake katika matini chanzi ni ile ile. Ujitokezaji huu wa maana nyingi tena mbadala unaibua sio tu uelewa mbadala bali pia ufasiri mbadala wa kisheria na kwa njia hiyo tafsiri inaishia kutatiza ufahamu wa lililokusudiwa. Maana ya kisheria pia inaishia kupotea katika kutafsiri huku. Kwa mfano, katika Sura ya 3, Kifungu cha 12;

**Kielelezo 21;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
12. <b>Entitlement</b> of citizens	<b>12. Haki</b> za raia

Neno *entitlement* kwa kadri lilivyotumiwa katika matini chanzi limebebehsa uelewa na fahiwa za kisheria/kikatiba, lakini neno hili limetafsiriwa kama haki. Neno *entitlement* kisheria linamaanisha kupewa haki kwa kuhistahiki haki hiyo kuhusiana na kitu fulani ambapo maana hii inaweza kurefushwa na kukajumuishwa maana kama vile ustabilifu wa haki kisheria. Haki nayo kwa Kiingereza inamaanisha *right* au *rights*. Kwa hivyo kutafsiri *entitlement* kama *rights* kunaleta ukinzani kwani istilahi hizi mbili hazina maana sawa. Katika sehemu inayofuata katika kifungu hicho cha 12, ibara ya (1) (a);

**Kielelezo 22;**

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
12. (a) the <b>rights, privileges and benefits</b> of citizenship, subject to the limits provided or permitted by this constitution; and,	12. (a) anastahili kupata <b>haki, fursa</b> na <b>faida</b> kwa mujibu wa katiba hii; na

Tafsiri hii imeonyesha matumizi ya maana za kiisimu pale ambapo palipo na istilahi za kisheria zinazotarajiwa kuibua maana za kisheria. Katika matini ya *Constitution of Kenya 2010 –rights, privileges and benefits* - haki, fadhila na mafao. Maneno *rights, privileges and benefits* katika muktadha huu yameekezwa maana za kisheria zinazokiuka fahiwa za kiisimu. Ili kufikia kuibua maana na fahiwa za kisheria matini lengwa haina budi kutumia istilahi mbadala – haki, fadhila na mafao. Neno *fursa* na *faida* zimebebehsa maana za kiisimu na wala haziibui maana za kisheria zilizowekezwa katika maneno *privileges and benefits*. ‘Faida’ ni istilahi inayotumika kikawaida katika uwanja wa kibiashara kwa maana ya *profit* au *profits*. Tukitafsiri ‘fursa’ kwa Kiingereza itakuwa ‘**opportunity**’ na wala si ‘**benefits**’.

**Kielelezo 22;**

Kifungu cha 12, ibara ya (1);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(1) Every citizen <b>is entitled to</b> ;	(1) Kila raia;

Kifungu hiki kinapotafsiriwa, maneno, *is entitled to* hayajatafsiriwa kama *ana haki ya* kama tulivyotarajia kutokana na tafsiri ya awali lakini tunaona kwamba tafsiri yake imepuuzwa. Hii ni kinyume na kanuni za tafsiri za kisheria ambapo kila neno lazima litafsiriwe. Matokeo yake ni kwamba matini lengwa inakosa kuwa na athari iliyokusudiwa. Makosa katika kutafsiri neno hili *entitled* yamejitokeza katika Kifungu cha 15;

**Kielelezo 23;**

Kifungu cha 15, ibara ya (5);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(5) This article applies to a person as from the effective date, but any requirements that must be satisfied before the person is <b>entitled</b> to be registered as a citizen shall be regarded as having been satisfied irrespective of whether the person satisfied them before or after the effective date, or after the effective date, or partially before, and partially after, the effective date.	(5) Kifungu hiki kitatumika kwa mtu kuanzia tarehe ya kuanza kutumiwa kwa Katiba hii, lakini mahitaji yoyote ambayo ni lazima yatimizwe kabla ya mtu <b>anayestahili</b> kusajiliwa kama raia yatachukuliwa kama yaliyotimizwa pasi na kuzingatia iwapo mtu huyu aliyatimiza kabla au baada kutekelezwa kwa Katiba hii ya tarehe ya kuanza, au kwa kiwango fulani kabla au baada ya tarehe ya kutekelezwa.

Katika kifungu cha 15, ibara ya (5) *entitled* imetafsiriwa kama *anayestahili*. Neno hili *entitled* limebebishwa fahiwa za kisheria lakini katika kutafisiri kwake maana inayojitokeza ni ya kiisimu. *Anayestahili* kutokana na uelewa wetu ina maana ya *who deserves*. Iwapo mtu atasoma tu makala hii ya Kiswahili basi huenda akapata ujumbe usiowiana na ule uliopo katika matini chanzi.

**Kielelezo 23;**

Kifungu cha 12,

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(1) Every <b>citizen</b> is entitled to;	(1) Kila <b>raia</b> ;

**Kielelezo 24;**

Kifungu cha 14, ibara ya (3);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(3) Parliament may enact legislation limiting the effect of clauses (1) and (2) on the <b>descendants of Kenyan citizens</b> who are born outside Kenya.	(3) Bunge linaweza kutunga sheria kuwekea mipaka athari za ibara ya (1) na (2) <b>kwa raia wa Kenya</b> ambao wamezaliwa nje ya Kenya.

**Kielelezo 25;**

Kifungu cha 16;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<b>A citizen</b> by birth does not lose citizenship by acquiring the citizenship of another country.	<b>Mtu</b> ambaye ni raia kwa kuzaliwa hapotezi uraia wake kwa sababu ya kupata uraia wa nchi nyingine.

**Kielelezo 26;**

Kifungu cha 17, ibara ya (1) (a);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(1) (a) the <b>person</b> acquired the citizenship by fraud, false representation or concealment of any material fact	(1) (a) iwapo <b>mtu</b> alijipatia uraia huo kwa njia ya ulaghai, udanganyifu wa uwakilishi au kuficha ukweli unaotakikana.

Katika Vifungu vilivyoko hapo juu kuna tafsiri potovu inayojitokeza kuhusiana na neno raia. Neno *citizen* limetafsiriwa kama *raia* katika Kifungu cha 12. Katika Kifungu cha 14, ibara ya (3), *descendants of Kenyan citizens* imetafsiriwa kama *raia wa Kenya*. *Descendant* inamaanisha watu ambao wana uhusiano wa kiukoo na wananchi walio nchini Kenya na wala si raia. Tukitafsiri raia wa Kenya itakuwa *Kenyan citizens* na wala si *descendants of Kenyan citizens*. Katika Kifungu cha 16, *a citizen* imetafsiriwa kama mtu. Tafsiri ya *mtu* kama ilivyoonyeshwa katika kifungu cha 17, ibara ya (1) (a) ni *person*. Katika kifungu cha 38, ibara ya (2) (a), *citizen* imetafsiriwa kama *mwananchi*. Katika tafsiri hizi zote ni kwamba hakuna istilahi mwafaka iliyoteuliwa kuwakilisha dhana ileile. Vilevile kuna ukinzani unaojitokeza katika Kifungu cha 14, ibara ya (4) na Kifungu cha 12;



**Kielelezo 27;**  
Kifungu cha 12;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
<b>Citizenship</b>	<b>Uraia</b>

**Kielelezo 28;**  
Kifungu cha 14, ibara ya (4);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(4) A child found in Kenya who is, or appears to be, less than eight years of age, and whose <b>nationality</b> and parents are not known, is presumed to be a citizen by birth.	(4) Mtoto anayepatikana nchini Kenya ambaye anaonekana kuwa na umri wa chini ya miaka minane, na ambaye <b>uraia</b> wake haujulikani na pia wazazi wake hawajulikani, atachukuliwa kuwa raia kwa kuzaliwa.

Kanuni za tafsiri hueleza kwamba mtafsiri lazima awe na mazoea ya kutumia neno moja kuelezea istilahi fulani katika tafsiri nzima bila kutumia neno lingine mbadala. Haya yamekiukwa katika Kifungu cha 12 na Kifungu cha 14 ambapo ***citizenship*** na ***nationality*** zimetafsiriwa kama ***uraia*** ambayo inazua upotovu wa kimaana. Kifungu cha 14, ibara ya (4), ***nationality*** imetafsiriwa kama ***uraia***. ***Nationality*** ina maana ya ***utaifa*** na wala si ***uraia***. Tafsiri hii pia imepuuza dhana ya uakifishaji iliyotumika katika matini chanzi. Koma zimetumika katika kutenganisha vifungu vya maneno lakini mtafsiri hakuliangazia hili kikamilifu katika matini lengwa. Matokeo yake ni kwamba matini ile inaishia kukosa kuwa na athari zilizokusudiwa.

Vilevile hakuna mtindo sawa wa kutafsiri neno ***contemplated*** katika Sura ya 3. Neno hili limewekezwa maana tofauti za kiisimu na kukinzana na maana ya kisheria iliyowekezwa katika matini chanzi. Baadhi ya tafsiri hizi ni kama zifuatavyo;

Kifungu cha 17, ibara ya (2)

***Contemplated*** - inavyofikiriwa

Kifungu cha 19, ibara ya (3) (c)

***Contemplated*** - inayoelezwa

Kifungu cha 27, ibara ya (5)

***Contemplated*** - kuonyeshwa

Kifungu cha 27, ibara ya (8)

*Contemplated* - zinazokusudiwa

Kifungu cha 22, ibara ya (4)

*Contemplated* - zinazoangaziwa

Kutafsiri *contemplated* kama inavyofikiriwa ni upotoshi kwa sababu kufikiriwa ina maana ya *thought*. **Kuonyeshwa** ina maana ya *shown* nayo **kusudiwa** ni *intended*. *Contemplated* ina maana ya *kuangaziwa*. Tafsiri hizi zinaifanya Katiba kukosa maana yake kisheria na kuishia tu kuwasilisha maana za kiisimu.

**Kielelezo 29;**

Kifungu cha 17, ibara ya (d), (i) na (ii);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(d) (i) a <b>penalty</b> of at least seven years imprisonment may be <b>imposed</b> ; or (ii) a more severe <b>penalty</b> may be <b>imposed</b>	(d) (i) <b>amepewa adhabu</b> ya kifungo cha angalau miaka saba au zaidi; au (ii) <b>hukumu</b> kali zaidi inaweza <b>kutolewa</b> .

Katika Kifungu hiki pia kumekosekana mtindo sawa wa kutafsiri neno *penalty*. Katika ibara ya (d) (i), limetafsiriwa kama *adhabu* na katika ibara ya (d) (ii) neno *penalty* limetafsiriwa kwa kupewa maana ya *hukumu*.

**Kielelezo 30;**

Kifungu cha 17, ibara ya (1) (a);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(1) (a) the <b>person</b> acquired the citizenship by <b>fraud, false representation</b> or concealment of <b>any material fact</b>	(1) (a) iwapo <b>mtualijipatia</b> uraia huo kwa <b>njia ya ulaghai, udanganyifu wa uwakilishi</b> au kuficha <b>ukweli unaotakikana</b> .

Kanuni za kutafsiri hueleza kuwa pale ambapo hakuna neno ambalo linapatikana katika matini chanzi maelezo huweza kutumika. Hali hii huweza kuzua tafsiri potovu na kuifanya makala kupoteza wasifu wake kama makala ya kisheria na kuibua maana za kiisimu tu. Maelezo yametumika kueleza maana tofauti za maneno katika Kifungu cha 17, ibara ya (1) (a);

- (a) *By fraud*
- (b) *False presentation*
- (c) *Concealment of any material fact*

Istilahi hizi zimetafsiriwa kama ifuatavyo;

- a) *Kwa njia ya ulaghai,*
- b) *udanganyifu wa uwakilishi au*
- c) *kuficha ukweli unaotakikana*

Tafsiri inayojitokeza imechukua mwelekeo wa kimaelezo, ambapo maelezo yenyewe mbali na kuibua fahiwa tofauti za uelewa, kwa kweli hayaoani na maana zinazojitokeza katika matini chanzi ya Kiingereza. Japo inawezekana kuonyesha katika misingi ya kiisimu hasa kwa kutumia mkakati wa kutafsiri kwa kurudi nyuma-Kiswahili-Kiingereza, matokeo yake yanatupelekea mbali sana na uelewa wa kisheria uliokusudiwa;

- a) *kwa njia ya ulaghai - by way of fraud*
- b) *udanganyifu wa uwakilishi - deception of presentation*
- c) *kuficha ukweli unaotakikana - to conceal the truth required.*

Hivyo basi dhana ya *material fact*- pengine inayoweza kutafsiriwa kama *ukweli bainifu*, imebanwa na kwa njia hii kukiuka kanuni ya tafsiri juu ya ubanaji wa ukweli unaojidhihirisha katika matini chanzi. Matokeo ya ubanaji huu ni kwamba maana inayojitokeza katika *Katiba ya Kenya 2010* haina athari za kisheria.

**Kielelezo 31;**

Kifungu cha 15, ibara ya (5);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
5) This article applies to a person as from the <b>effective date</b> , but any requirements that must be satisfied before the person is <b>entitled</b> to be registered as a citizen shall be regarded as having been satisfied irrespective of whether the person satisfied them before or after the <b>effective date</b> , or after the effective date, or <b>partially</b> before, and partially after, the <b>effective date</b> .	(5) Kifungu hiki kitatumika kwa mtu kuanzia <b>tarehe ya kuanza kutumiwa kwa Katiba hii</b> , lakini mahitaji yoyote ambayo ni lazima yatimizwe kabla ya mtu <b>anayestahili</b> kusajiliwa kama raia yatachukuliwa kama yaliyotimizwa pasi na kuzingatia iwapo mtu huyu aliyatimiza kabla au baada ya <b>tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii</b> , au kwa <b>kiwango fulani</b> kabla au baada ya <b>tarehe ya kutekelezwa</b> .

Mojawapo ya wasifu wa matini za kisheria ni matumizi ya sentensi ndefu. Mtafsiri anapotafsiri sentensi hizi huweza kukumbana na changamoto za kuhawilisha mawazo yote yaliyomo katika matini chanzi hadi matini lengwa. Kwa mfano Kifungu cha 15, ibara ya (5) kimekumbwa na changamoto wakati wa kutafsiri. Kwanza, *effective date* ina maana ya kisheria iliyowekezwa ndani yake lakini inatafsiriwa kwa maelezo kama *tarehe ya kuanza kutumiwa kwa Katiba hii*. Kwa Kiingereza hii ina maana ya *before the date of the use of this Constitution* ambayo ni tofauti na ile iliyoko katika matini chanzi. Pili, *effective date* inatafsiriwa kama *tarehe ya kuanza kutekelezwa kwa Katiba hii*. Kwa Kiingereza hii ina maana ya *before the date of the implementation of this Constitution*. Kisha mwishowe inatafsiriwa kama *tarehe ya kutekelezwa* ambayo kwa Kiingereza ina maana ya *the date of the implementation*. Tafsiri hizi zinaonyesha kukinzana kwa maana ya maneno yaleyale yaliyomo katika matini chanzi.

Vilevile katika Vifungu vifuatavyo ukinzani wa maana umejitokeza kutokana na tafsiri potovu hasa ambayo inatokana na maelezo. Kwa mfano;

**Kielelezo 32;**

Kifungu cha 13, ibara ya (1);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
13. (1) Every person who was a citizen immediately before the <b>effective date</b> retains the same citizenship status <b>as of that date</b>	13. (1) Kila mtu ambaye alikuwa raia punde tu kabla ya <b>kuanza kutumika Katiba hii</b> atadumisha hali ya uraia wake

**Kielelezo 33;**

Kifungu cha 14, ibara ya (2);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
14. (2) Clause (1) applies equally to a person born before <b>the effective date</b> , whether or not the person was born in Kenya, if either the mother or father of the person is or was a citizen.	14. (2) Ibara ya (1) itatumika sawa kwa mtu ambaye alizaliwa <b>kabla ya siku ya kuanza kutumika</b> kwa Katiba hii, iwe amezaliwa nchini au la, ikiwa mama au baba yake ni, au alikuwa raia.

Katika Vifungu hivi, kumetokea ukinzani wa maana wakati wa kutafsiri kutoka MC hadi ML. Katika Kifungu cha 13, ibara ya (1), *effective date* inatafsiriwa kama *kuanza kutumika katiba hii*. Tafsiri ya *tarehe* haijaonyeshwa popote katika ML. Hili linakiuka kanuni ya kutafsiri matini za kisheria ambapo kila neno ni lazima litiliwe maanani wakati

wa kutafsiri. Kifungu hiki pia kinatafsiri ya *status as of that date* kama *hali ya uraia wake*. Tafsiri hii ingekuwa *hadhi ya uraia wake kama vile ingekuwa tarehe hiyo*. Katika Kifungu cha 14, ibara ya (2), *effective date* imetafsiriwa kama *kabla ya siku ya kuanza kutumika kwa katiba hii*. *Date* ni *tarehe* na wala sio *siku* kama ilivyotafsiriwa hapa. Tafsiri hizi zinajitokeza kwa sababu ya kutumia maelezo ya kiisimu kuelezea maneno yenye fahiwa za kisheria.

**Kielelezo 34;**

Kifungu cha 17;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
17. <b>Revocation</b> of citizenship	17. <b>Kupokonywa</b> uraia

Maneno ya kisheria yenye fahiwa na maana za kisheria hayawezi kutafsiriwa kwa kutumia maneno ya kawaida. Hali hii huweza kuzua tafsiri potovu ambayo inawakilisha maana za kiisimu. Hili limejitokeza pale ambapo *revocation* inatafsiriwa kama *kupokonywa*. *Revocation* ina maana ya *ubatilishaji wa makubaliano kuhusu kitu au jambo kati ya watu au makundi mawili*. *Kupokonywa* inapotumika huwa na maana ya *kuchukua kitu kutoka kwa mtu na hasa bila idhini yake* na kwa Kiingereza ina maana ya *deny*. Lakini katika muktadha huu *revocation* ina maana ya *ubatilishwaji wa makubaliano yaliyokuwepo wakati wa kujisajili kama raia wa nchi ya Kenya*. Kutafsiri istilahi hii kama *kupokonywa* basi kunaleta utata na ukinzani wa maana. Hili linaweza kuzua utata kwa wasomaji wa Katiba hii hasa katika kuelewa yale yaliyokusudiwa.

**3.3 Hitimisho**

Katika sura hii tulichanganua data na kuonyesha changamoto zinazojitokeza katika kutafsiri Sura ya 3 ya *Constitution of Kenya 2010*. Changamoto hizi zinatokana na ukosefu wa kuzingatia usawidi wa kisheria wakati wa kufanya tafsiri. Tulionyesha baadhi ya mikinzano ya kimaana inayojitokeza na palipowezekana tulitoa tafsiri ambayo ingefaa kutumika.

## SURA YA NNE

### TATHMINI YA SURA YA 4 YA *CONSTITUTION OF KENYA 2010*

#### **4.0 Utangulizi**

Katika sura hii, tulichanganua data kutoka Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010* kwa kuilinganisha katika viwango mbalimbali na tafsiri yake ya Kiswahili *Katiba ya Kenya 2010*. Uchanganuzi uliofanywa ulidhamiria kubainisha ulinganifu wa kimaana wa maneno, istilahi za kisheria na vifungu vya kisheria kwa kadri vilivyotafsiriwa kwa Kiswahili. Kulifanywa mijadala kadha wa kadha kuzungumzia kanuni za kutafsiri zinazohusika pale ambapo panadhihirika kwamba yapo makosa, utata, utohakika na ukiukaji wa kimaana, upotoshi wa taratibu za usawidi wa kisheria na masuala mengine sawia na hayo katika tafsiri za vifungu au ibara mahususi kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Pale ilipowezekana, tumejaribu kuonyesha ni kwa nini makosa mahususi yalijitokeza na pia tumependekeza jinsi tafsiri hizo zilivyofaa kushughulikiwa ili kuyabana makosa hayo.

#### **4.1 Ufafanuzi wa Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010***

Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010* inahusu Sheria ya Haki. Sehemu hii inatoa maelezo na masharti ya kijumla kuhusu haki na uhuru wa kimsingi na utekelezaji wa haki hizi. Mahakama kuu ina mamlaka kuhakikisha kuwa haki hizi hazijukiukwa na kuamua kesi inayohusu kunyimwa, kukiukwa au kusitishwa kwa haki au uhuru wa kimsingi. Kila mtu ana haki ya kuishi na kila mtu ni sawa kisheria. Kila mtu ana haki ya uhuru na usalama wake, ana haki ya faragha yake, haki ya uhuru wa kujieleza, haki ya kupata habari ilizonazo serikali na haki katika kusikizwa kesi. Baadhi ya uhuru alionao raia yeyote ni kama vile uhuru wa kutangamana na uhuru wa kutembea na uhuru wa kuwa na makaazi. Tume ya Haki za Binadamu na Usawa imeundwa ili kuimarisha na kulinda uzingativu wa haki za binadamu katika taasisi zote. Malengo ya Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya* ni kufahamisha wananchi kuhusu haki zao na kuzilinda zisije zikakiukwa.

#### **4.2 Ukinzani wa Maana Unaojitokeza katika Kutafsiri Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010***

Lengo la *Constitution of Kenya 2010* hasa Sura ya 4 ni kuwasilisha ujumbe muhimu sheria ya haki kwa wananchi wake. *The Constitution of Kenya 2010* iliyotafsiriwa kama *Katiba ya Kenya 2010* imetafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili na katika kutafsiriwa kwake kunajitokeza makosa ya ukosefu wa ulinganifu wa maana katika

misingi ya kiisimu na kisheria hali kadhalika kunajitokeza ukinzani wa maana hasa za kisheria. Matini lengwa ambayo ni *Katiba ya Kenya 2010* kwa lugha ya Kiswahili inaishia kupoteza maana ya kisheria na kuwasilisha maana za kiisimu pale ambapo kunatarajiwa kujitokeza sio tu maana ya maneno na istilahi za kisheria bali pia uelewa wa kisheria. Moja kati ya kanuni na mhimili wa nadharia ya *Skopos* ni kuwepo kwa kauli kwamba kila matini inayotafsiriwa huwa na lengo mahususi linalokusudiwa kutekelezwa katika miktadha lengwa na lazima lengo hili litimizwe. Lazima pia mtafsiri ahakikishe kuwa matini chanzi ina mshikamano na matini lengwa na kuna uwiano.

Kanuni ya tafsiri hueleza kuwa kila neno linalojitokeza katika matini chanzi lazima itafsiriwe katika matini lengwa. Kama neno lipo katika hali ya umoja litafsiriwe kwa umoja na kama ni wingi vilevile itafsiriwe vivyo hivyo.

**Kielelezo 35;**

Kifungu cha 36, ibara ya (1);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
36. (1) Every person has the right to freedom of association, which includes the <b>right to form</b> , join or participate in the activities of an <b>association of any kind</b> .	36. (1) Kila mtu ana haki ya uhuru wa kutangamana ambayo imahusu <b>haki ya kuanzisha</b> , kujiunga na, au kushiriki katika majukumu ya <b>mashirika</b> .
(2) A person shall not be compelled to join an <b>association of any kind</b> .	(2) Mtu hatalazimishwa kujiunga na <b>muungano wa aina yoyote</b> .
(3) Any legislation that requires registration of an <b>association of any kind</b> shall provide that-	(3) Sheria yoyote kuhusu usajili wa <b>miungano ya makundi ya kijamii</b> itahitaji kwamba-

Mojawapo ya kanuni za tafsiri ni kuwa neno linapotumika sana katika matini nzima ni vema kutumia maelezo sawa kuelezea neno lile. Mtafsiri anapobadilisha jinsi anavyoelezea dhana ileile basi inaonyesha kwamba hajaimarika katika kufanya tafsiri ile. Katika ibara ya (1), *association of any kind* imetafsiriwa kama *mashirika*. Mashirika ina maana ya *organizations* na wala si *association*. Vilevile, haifai kuwa *mashirika* kwani tunazungumzia *association* na wala si *associations*. Katika ibara ya (2), *association of any kind* imetafsiriwa kama *muungano wa aina yoyote*. Na mwishowe katika ibara ya (3), *association of any kind* imetafsiriwa kama miungano ya makundi ya kijamii.

Makundi ya kijamii ina maana ya *societal/social groups*. *Association* ina maana ya muungano lakini katika kutafsiri kwake neno hili limeelezwa kwa wingi badala ya umoja. Pia muungano huu hatujaelezwa ni wa aina gani basi inafaa tafsiri yake iwe *muungano wa aina yoyote* kama ilivyo katika ibara ya (2). *Association of any kind* imetafsiriwa kwa maelezo tofauti katika ibara zote mbili na hivyo basi kuzua utata kuhusu uelewa wa maneno haya.

**Kielelezo 36;**

Kifungu cha 20, ibara ya (4);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
20. (4) In interpreting the Bill of Rights, a court, <b>tribunal</b> or other <b>authority shall promote-</b>	20. (4) Katika kufasiri Sheria ya Haki, mahakama, <b>mahakama maalum</b> , au <b>mamlaka</b> nyingine <b>zitaendeleza-</b>

**Kielelezo 37;**

Kifungu cha 23, ibara ya (2);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
23. (1) <b>The High court</b> has <b>jurisdiction</b> , in accordance with Article 165, to hear and determine applications for redress of a denial, violation or infringement of, or threat to, a right or a fundamental freedom in the Bill of Rights.	23. (1) <b>Mahakama Kuu</b> ina <b>mamlaka</b> kwa mujibu wa Kifungu cha 165 kusikiliza upya na kuamua kesi inayohusu kunyimwa, kukiukwa, kuvunjwa au kutishiwa kwa haki au uhuru wa kimsingi katika Sheria ya Haki.
(2) Parliament shall enact legislation to give original jurisdiction in appropriate cases to <b>subordinate courts</b> to hear and determine applications for redress of a denial, violation or infringement of, or threat to, <i>a right or fundamental freedom</i> in the Bill of Rights.	(2) Bunge litatunga sheria kutoa uwezo wa kiasili kwa <b>mahakama ya chini</b> katika kusikizwa upya na kuamuliwa kwa kesi dhidi ya kunyimwa, kuvunjwa na kukiukwa kwa Sheria ya Haki.

Maelezo yanapotumika katika kuelezea istilahi za kisheria, huweza kukatokea maana za kiisimu tu ambazo hazibebi maana kisheria. Katika Kifungu cha 20, ibara ya (4) maelezo yametumika kueleza maana ya *tribunal* ambayo inalezwa kama *mahakama maalum*. Hii ni tafsiri potovu kwani tukitafsiri kurudi nyuma itakuwa *special court* na wala si *tribunal*. Katika Kifungu cha 23, ibara ya (2), *subordinate court* inaelezwa kama *mahakama ya chini*. *Mahakama kuu* katika Kifungu cha 23, ibara ya (1) imetajwa kama *High court*.



**Jurisdiction** ambayo ni neno lililobebeshwa maana kisheria inaelezewa kwa neno la kawaida kama **mamlaka**. Neno hili lingetafsiriwa kama **mamlaka ya kisheria**. Maana hizi zinaibua matini ambayo haina athari za kisheria kwa inatumia maana za kiisimu. Katika ibara ya (2), **a right or fundamental freedom** ni maneno ambayo hayajahawilishwa katika ML. Tafsiri yake ilifaa kuwa **haki na uhuru wa kimsingi**. Kila neno ni lazima lifanyiwe tafsiri na hili lisipofanywa basi kunatokea ukinzani wa maana iliyowasilishwa katika MC na ile iliyoko katika ML.

**Kielelezo 38;**

Kifungu cha 22, ibara ya (3) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(b) formalities relating to <b>the proceedings</b> , including commencement of the <b>proceedings</b> , are kept to the minimum, and in particular that the court shall, if necessary, <b>entertain proceedings</b> on the basis of <b>informal documentation</b> ;	(b) urasmi unaohusiana na <b>kesi hizo</b> , kukiwemo kuanzishwa kwa <b>kesi</b> , unawekwa kwa kiwango cha chini, na hasa pakiwa na haja, mahakama <b>itakubali kuwepo kwa kesi</b> kwa misingi ya <b>rekodi zisizo na ulazima wa urasmi</b> .

Kanuni ya kutafsiri huruhusu kutumika kwa maelezo pale ambapo neno mbadala limekosekana katika lugha lengwa. Hata hivyo hili linapofanyika lazima mtafsiri ahakikishe kuwa lengo la matini ile haijapotoka. Katika kutafsiri matini ya kisheria lazima mtafsiri azingatie usawidi wa kisheria kila wakati. Katika Kifungu cha 22, ibara ya (3) (b) kuna hali ya ukinzani inayojitokeza pale ambapo **informal documentation** inatafsiriwa kama **rekodi zisizo na ulazima wa urasmi**. Haya ni maelezo ambayo hayaafiki tafsiri ambayo imetolewa kwa Kiingereza. **Informal documentation** ingetafsiriwa kama **hati isiyorasmi**. Tafsiri hii pia imekosa kulenga usawidi wa kisheria pale ambapo **proceedings** ambayo ina fahiwa za kisheria inatafsiriwa kama **kesi** na pia **entertain proceedings** inapewa maana ya **itakubali kuwepo kwa kesi**.

**Kielelezo 39;**

Kifungu cha 38, ibara ya (2);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) Every adult citizen has the right, without <b>unreasonable restrictions</b> -	(2) Kila raia akiwa mtu mzima ana haki <b>pasipo na masharti yasiyo na busara-</b>

Vilevile tafsiri iliyotolewa katika Kifungu cha 38, ibara ya (2) inatumia maelezo. *Unreasonable restrictions* imetafsiriwa kama *pasipo na masharti yasiyo na busara*. Maelezo yaliyotolewa hayashikamani na maelezo yaliyo katika MC. Hili linatokea kwa sababu ya ukosefu wa istilahi mwafaka inayoafiki istilahi zilizotumika na hivyo kutumia maelezo ambayo yanaleta ukinzani wa kimaana. *Unreasonable restrictions* ina maana ya *vizuizi visivyo vya busara. Every adult citizen* pia imetafsiriwa kwa njia potovu kama *kila raia akiwa mtu mzima*. Maana hii haijahawilisha ujumbe uliopo katika MC kwa sababu hatujaelezwa kuhusiana na *raia akiwa mtu mzima* bali tumeelezwa kuhusiana na *raia watu wazima*.

**Kielelezo 40;**  
Kifungu cha 30,

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
30. <b>Slavery, servitude and forced labour</b>	30. <b>Utumwa na kazi ya kulazimishwa</b>

Tafsiri za kisheria zinapofanywa ni muhimu kuhakikisha hakuna neno lolote au kifungu chochote ambacho kinaachwa bila kutafsiriwa. Ni bayana kuwa katika matini chanzi kuna istilahi *slavery* na *servitude* ambazo zinatafsiriwa kwa pamoja kama *utumwa*. Katika MC haiwezi ikawa kwamba kuna urudiaji ambao ulijitokeza hapa na kila neno lazima kuna maana iliyokusudia kuwakilisha. Lakini kwenye ML istilahi mwafaka ya kuwasilisha istilahi hizo mbili ikawa ni vigumu kupata kwani maneno haya mawili yanakaribiana sana kimaana kama *utumwa*. Tafsiri hii inakiuka kanuni za tafsiri za kisheria ambazo huhitaji kila neno litafsiriwe na hata kama kuna urudiaji ni lazima urudiaji huo uonyeshwe kwa sababu kila neno huwa na umuhimu wake. Kuachwa kwa maneno bila kutafsiriwa kunaleta maana potovu hasa kwa raia watakaoisoma Katiba hiyo.

Vilevile katika kutafsiri sheria ni muhimu kuhakikisha kuwa hakuna maneno yatakayoongezwa katika ML ambayo hayamo katika MC. Hili likifanyika basi kutakuwa hakuna uwiano kati ya MC na ML na hili litasababisha ukinzani. Kwa mfano;

**Kielelezo 41;**

Kifungu cha 24, ibara (2) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
24. (2) (b) <b>shall not be construed</b> as limiting the right or fundamental freedom unless the <b>provision</b> is clear and specific about the right or freedom to be limited and the nature and extend of the limitation; and	24. (2) (b) <b>halitachukuliwa</b> kama kuzuia haki au uhuru <b>uliotajwa katika Sheria ya Haki</b> isipokuwa pale ambapo <b>sharti</b> hilo linaeleza wazi na kwa yakini kuhusu haki

**Kielelezo 42;**

Kifungu cha 24, ibara ya (2) (c);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
24. (2) (c) shall not limit the right of fundamental freedom <b>so far</b> as to <b>derogate</b> from its core or <b>essential content</b>	24. (2) (c) halitazuia haki au uhuru wa kimsingi <b>unaotajwa katika Sheria ya Haki</b> ili <b>kupunguza uzito</b> na umuhimu uliowekwa katika <b>haki hiyo</b> .

Katika Kifungu cha 24, ibara ya 24 (b), *uliotajwa katika sheria ya Haki* ni maneno ambayo yameongezwa katika ML na hayamo katika MC. Kuongezwa kwa maneno katika tafsiri ni jambo lisiloepukika katika tafsiri za kisheria lakini hili halifai kubadilisha maana iliyokusudiwa kwa vyovyote vile. Maneno yaliyoongezwa yanafaa tu kuhawilishwa maana katika matini chanzi na wala si kuibadilisha. Katika Kifungu cha 24, ibara ya (2) (c) vilevile maneno, *unaotajwa katika sheria ya Haki* yameongezwa. Kuongezwa kwa maneno ambayo hayajitokezi katika MC kunakiuka kanuni za tafsiri kwani mtafsiri anafaa kutafsiri matini chanzi bila kuongeza wala kupunguza chochote na akifanya hivi kunatokea ukinzani wa kimaana kati ya MC na ML. *So far* kwa maoni yetu ingetafsiriwa kama *ulioangaziwa*. *Essential content* pia imetafsiriwa kama *haki hiyo*. *Haki hiyo* tukitafsiri kwa Kiingereza tena itakuwa *that right* na wala si *essential content*. Maana ya *essential content* labda ingekuwa *maudhui muhimu*. Mtafsiri hapa amebadilisha maana ya MC na hivyo kuzua tafsiri potovu.

**Kielelezo 43;**

Kifungu cha 20, ibara ya (2);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
20. (2) Every person <b>shall enjoy</b> the rights and fundamental freedoms <b>in the</b> Bill of Rights in the greatest extent consistent with the <b>nature</b> of the right or <b>fundamental freedom</b> .	20. (2) Kila mtu <b>ana</b> haki na uhuru wa kimsingi <b>uliotajwa katika</b> Sheria ya Haki, kwa kiwango kikubwa kuambatana na <b>hali</b> ya haki hiyo au <b>uhuru huo wa kimsingi</b> .

**Kielelezo 44;**

Kifungu cha 20, ibara ya (5) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(5) (b) in allocating resources, the State <b>shall give priority</b> to ensuring the <b>widest possible enjoyment</b> of the right or fundamental freedom having <b>regard to prevailing circumstances</b> , including the <b>vulnerability of particular</b> groups or individuals; and	(5) (b) katika kugawa rasilmali, Serikali <b>ina jukumu</b> la kuhakikisha kuwa <b>uwezekano mkubwa wa kunufaishwa</b> na haki au uhuru wa kimsingi kwa <b>kuzingatia hali halisi</b> , kukiwemo <b>kutengwa kwa baadhi</b> ya makundi au watu binafsi; na

**Kielelezo 45;**

Kifungu cha 24, ibara ya (1) (d);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
24. (1) (d) the need to ensure that the <b>enjoyment of rights</b> and fundamental freedoms by any individual <b>does not prejudice</b> the rights and fundamental freedoms of others; and	24. (1) (d) haja ya kuhakikisha kuwa <b>kufurahia wa haki hizo</b> na uhuru huo wa kibinafsi kwa mtu yeyote <b>hautatizi</b> haki na uhuru wa kimsingi wa watu wengine; na

Matini za kisheria huhitaji mtafsiri kuwa makini anapotafsiri kwani maneno ya kawaida yanaweza kutumika katika muktadha wa kisheria na kubebeshwa maana tofauti ambayo inatarajiwa aizingatie anapotafsiri. Katika Katiba pia kuna matumizi ya maneno ya kawaida ambayo yana maana tofauti kisheria. Kwa mfano katika Kifungu cha 20, ibara ya (2), *shall enjoy the rights* ni maneno yaliyotumika katika MC ambayo yametafsiriwa kama *ana haki* katika ML. Kifungu cha 24, ibara ya (1) (d), tafsiri ya *enjoyment of rights* ni *kufurahia wa haki*. Katika Kifungu cha 20, ibara ya (5) (b), *widest possible enjoyment* imetafsiriwa kama *uwezekano mkubwa wa kunufaishwa*. Hapa mtafsiri anaonekana kutoa maana tofauti kuhusu *enjoyment*. *Kunufaishwa* kwa mfano imetokana

na neno *nufaika* ambayo hutumika sana katika biashara kumaanisha *kupata faida*. Katika tafsiri hizi maana ya kawaida ya *enjoyment* ambayo ni *kufurahia* ndiyo iliyotumika. Mtafsiri hakuzingatia maana ya neno kwa kulenga kuafiki matarajio ya usawidi wa kisheria. Maana ya *enjoyment* kisheria ina maana ya *kutekelezwa kwa haki* na kwa uelewa huo *enjoyment* ni *kuridhia haki* wala si *kufurahia*. Katika matini za kisheria ni muhimu mtafsiri azingatie maana za kisheria na wala si maana za kawaida pekee. Maneno *does not prejudice* yamebebehsa maana za kisheria lakini katika ML yanatafsiriwa kama *hautatizi*. Tafsiri hii inakosa kuibusha dhana ya kisheria katika ML na hivyo kuzua tafsiri iliyobebeshwa fahiwa za kiisimu.

**Kielelezo 46;**

Kifungu cha 21, ibara ya (3);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(3) All State organs and all <b>public officers</b> have the duty to address the needs of the <b>vulnerable groups</b> within society, including women, <b>older members of society</b> , persons with disabilities, children, youth, <b>members of minority</b> or <b>marginalized</b> communities, and <b>members</b> of particular ethnic, religious or cultural communities.	(3) <b>Ni wajibu wa</b> mashirika yote ya Serikali na <b>watumishi</b> kushughulikia mahitaji ya <b>makundi maalum</b> katika jamii, wakiwemo wanawake, <b>wazee</b> , watu wenye ulemavu, watoto, vijana na <b>jamii za walio wachache</b> au <b>zilizotengwa</b> , pamoja na <b>jamii</b> fulani za kikabila, kidini na kitamaduni.

**Kielelezo 47;**

Kifungu cha 22, ibara ya (2) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(b) a person <b>acting as a member of</b> , or in the interest of, a group or a class of persons;	(b) mtu <b>ambaye pia ni mwanachama wa kundi fulani</b> au kwa hiari ya kundi au tabaka fulani la watu;

Katika Kifungu cha 21, ibara ya (3), *vulnerable groups* imetafsiriwa kama *makundi maalum*. Tafsiri hii ina ukinzani kwa sababu *makundi maalum* kwa Kiingereza ni *special groups* na wala si *vulnerable groups*. *Vulnerable* ina maana ya kuwa katika hali ya kuweza kuadhirika, kwa hivyo *vulnerable groups* ni makundi ya wale wanaoweza kudhuriwa. *Older members of society* imetafsiriwa kama *wazee*. Tafsiri ya *older members of society* kwa Kiswahili kwa uelewa wetu yafaa kuwa *wakongwe katika jamii*.

Vilevile ukinzani wa kimaana unajitokeza pale ambapo *members of minority* imetafsiriwa kama *jamii za walio wachache*. *Jamii* kwa Kiingereza ni *society*. Tafsiri ya *members* inafaa kuwa *wanachama* kama ilivyo katika Kifungu cha 22, ibara ya (2) (b). Tafsiri hii basi inafaa kuwa *walio wachache*. Iwapo istilahi haijatafsiriwa sawa basi uwiano kati ya MC na ML unakuwa haupo. Ukinzani huu unatokea hasa kwa sababu ya mtafsiri kukosa kutumia istilahi bora kabisa katika ML inayolingana kimaana na istilahi iliyotumika katika MC na katika hali ile maana inapotoka.

**Kielelezo 48;**

Kifungu cha 24, ibara ya (5) (c);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(5) (c) Article 37- Assembly, demonstration, <b>picketing</b> and <b>petition</b> ;	(5) (c) Kifungu 37- Mikutano, maandamano, <b>migomo</b> na <b>malalamiko</b> ;

Katika Kifungu cha 24, ibara ya (c) kuna tafsiri potovu inayojitokeza. *Picketing and petition* imetafsiriwa kama *migomo na malalamiko*. Migomo inatokana na ‘goma’ ambayo ina maana ya kusimama kidete na kuamua kutoenda kazini hadi haki za waliogoma zisikizwe. *Picketing* nayo kwa upande mwingine ni ile hali ya watu kujitokeza na kushawishi wengine ili wagome. *Petition* nayo ni istilahi ya kisheria ambayo ina maana ya ombi la haki na maana hii inakinzana na iliyotumika ya malalamiko. Tafsiri iliyotumika ya *migomo* na *malalamiko* haiibui dhana ya kisheria kama ilivyo katika MC. Maana inayojitokeza inaonekana kuwa ya kawaida.

**Kielelezo 49;**

Kifungu cha 20, ibara ya (4) (a);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(a) the values <b>that underlie</b> an open and democratic society based on <b>human dignity</b> , equality and freedom; and	(a) maadili <b>yanayoongoza</b> jamii iliyo wazi na ya kidemokrasia kulingana na <b>heshima ya ubinadamu, ulinganifu, usawa, na uhuru</b> ; na

**Kielelezo 50;**

Kifungu cha 28;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
28. <b>Human dignity</b> Every person has <b>inherent dignity</b> and the right to have <b>that dignity</b> respected	28. <b>Hadhi ya binadamu</b> Kila mtu <b>anamiliki heshima ya kuzaliwa kama binadamu</b> na haki ya kutaka <b>hali</b>

and <b>protected</b> .	<b>hii iheshimiwe</b>
------------------------	-----------------------

Kifungu cha 20, ibara ya (4) (a), *human dignity* imetafsiriwa kama *heshima ya ubinadamu*. Heshima inatafsiriwa kama *respect* kwa lugha ya Kiingereza. *Dignity* ina maana ya hadhi kama ilivyotafsiriwa katika Kifungu cha 28. Kifungu hiki kina ukinzani wa maana pale ambapo *inherent dignity* inatafsiriwa kama *anamiliki heshima ya kuzaliwa kama binadamu*. Maelezo haya katika ML yanakinzana kimaana na yale yaliyopo katika MC. *Inherent* ina maana ya *kiasili* na *dignity* ni *hadhi*. Katika kifungu hiki *that dignity* imerejelewa kama *hali hii*. Mtafsiri angefaa kurudia tena tafsiri hii kama *hadhi hiyo*. Mojawapo ya wasifu wa kisheria ni urudiaji na hili lazima lionyeshwe katika ML kwa kurudia kinyume na kufanya hivi matini ile itapoteza wasifu wake kama matini ya kisheria Mwishowe ukinzani unajitokeza pale ambapo *protected* imetafsiriwa kama *iheshimiwe*. Maana ya *protected* ni *kulindwa*. *Iheshimiwe* ina maana ya *to be respected*.

**Kielelezo 51;**

Kifungu cha 37;

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
37. Every person has the right, <b>peaceably and unarmed</b> , to assemble, to demonstrate, <b>to picket</b> , and to present petitions to public authorities.	37. Kila mtu ana haki, <b>bila haja ya kuomba ruhusa</b> , ya kukutana, kuandamana, <b>kugoma</b> , na kuwasilisha malalamiko yake kwa mamlaka ya umma ila tu afanye hivyo kwa amani na bila kutumia silaha.

**Kielelezo 52;**

Kifungu cha 38, ibara ya (2) (b);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(2) (b) <b>any office</b> of any political party of which the citizen is a member.	(2) (b) <b>kiongozi wa afisi</b> yoyote ya chama cha kisiasa ambacho mwananchi huyo ni mwanachama.

Ukosefu wa uwiano wa kimaana unajitokeza katika Kifungu cha 37, pale ambapo *peaceably and unarmed* inatafsiriwa kama *bila haja ya kuomba ruhusa*. Tukitafsiri kwa Kiingereza *bila haja ya kuomba ruhusa* itakuwa *without necessity to request for permission*. *Peaceably and unarmed* ina maana ya *kwa amani na bila silaha yoyote*. Tafsiri hii hailingani kabisa na MC na hivyo kuzua ukinzani wa kimaana. Katika Kifungu cha 38, ibara ya (2) (b), *any office* inatafsiriwakama *kiongozi wa afisi yoyote*. *Kiongozi*

*wa afisi yoyote* kwa kiingereza ina maana ya *a leader of any office. Any office* tafsiri yake ni *afisi yoyote*. Tafsiri potovu inapofanywa maana kusudiwa inakosa kufikia wasomaji na hivyo basi matatizo yanajitokeza katika utekelezaji wake. Utata huu unapojitokeza itabidi wasomaji kurejelea MC ili kupata maana sawa.

**Kielelezo 53;**

Kifungu cha 49, ibara ya (1) (a);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
49. (1) (a) <b>to be informed promptly</b> , in language that the person understands, of-	49. (1) (a) <b>kuarifiwa kwa upole</b> na kwa lugha anayoielewa, kuhusu-

Kifungu cha 49, ibara ya (1) (a), *to be informed promptly* imetafsiriwa kama *kuarifiwa kwa upole*. Maelezo haya yanakinzana na yale ya MC. *To be informed promptly* imetafsiriwa kama *moja kwa moja* kama ilivyo katika Kifungu cha 50, ibara ya (2) (h) ambayo pia inazua tafsiri potovu. *To be informed promptly* ingefaa kuwa *kuarifiwa mara moja* au *kuarifiwa papo hapo*. Katika Kifungu cha 50, ibara ya (2) (l), pia kuna tafsiri potovu inayojitokeza;

**Kielelezo 54;**

Kifungu cha 50, ibara ya (2) (l);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
50. (2) (l) <b>to refuse to give self-criminating evidence;</b>	50. (2) (l) <b>kutolazimishwa kutoa ushahidi wa kujifunga;</b>
2 (h) to have an advocate assigned to the accused person by the State and at State expense, if <b>substantiatial injustice would otherwise result</b> , and to be informed of this right <b>promptly;</b>	(2) (h) kuwa na wakili aliyetolewa na Serikali kwa gharama ya Serikali yenyewe, <b>endapo haki yake ya msingi imevunjwa</b> , na aathiriwe kuhusu haki hii <b>moja kwa moja;</b>

*To refuse* ina maana ya *kukataa kufanya jambo*. Maneno haya kutafsiriwa kama *kutolazimashwa* basi kunaleta ukinzani wa kimaana. *Kutolazimishwa* kwa Kiingereza ina maana ya *not to be compelled. To refuse to give self-criminating evidence* inafaa kutafsiriwa kama *kukataa kutoa ushahidi wa kujitia hatiani au ushahidi wa kujiponza*. Kanuni ya kutafsiri matini ya kisheria ni kuwa neno litafsiriwe jinsi lilivyo na mabadiliko yoyote yasifanywe wakati wa kutafsiri.



**Kielelezo 55;**

Kifungu cha 19, ibara ya (3);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
(3) The rights and fundamental freedoms <b>in the Bill of Rights-</b>	(3) Haki na uhuru wa kimsingi <b>zinazotajwa katika sura hii-</b>
(3) (b) <b>do not exclude</b> other rights and fundamental freedoms <b>not in the Bill of Rights</b> , but recognized or conferred by law, except to the extent that they are inconsistent with this Chapter; and	(3) (b) <b>hazitengi</b> haki na uhuru mwingine wa kimsingi ambao <b>haukutajwa katika Sura hii</b> , lakini zinazotambuliwa na kukubaliwa na sheria ila kwa kiwango ambacho hazikubaliani na Sura hii, na

Ukinzani wa maana kisheria unajitokeza pia iwapo kuna kifungu katika MC ambacho kimerejelewa lakini katika ML kinakosa kutajwa na mtafsiri anatumia viwakilishi kukiwakilisha. Katika hali hii viwakilishi vinatumika kuwakilisha istilahi au vifungu vilivyorudiwa. Kwa mfano katika Kifungu cha 19, ibara ya (3), **the rights and fundamental freedoms in the Bill of Rights** imetafsiriwa kama **Haki na uhuru wa kimsingi zinazotajwa katika sura hii**. Katika MC tumetajiwa **the bill of rights** na wala si **this chapter** kama ilivyotafsiriwa kwa Kiswahili. Vilevile, katika Kifungu hicho cha 19, ibara ya (3), do not exclude other rights and fundamental freedoms not in the Bill of Rights imetafsiriwa kama **hazitengi haki na uhuru mwingine wa kimsingi ambao haukutajwa katika sura hii**. Katika vifungu hivi kuna chukulio kwamba tunajua Sura hii inahusu nini na badala ya mtafsiri kuitaja moja kwa moja anatumia viwakilishi. Kanuni mojawapo ya kutafsiri ni kwamba ni lazima kila neno litafsiriwe hata kama kuana urudiaji unaojitokeza lazima hili lionyeshwe kwani ni sifa kuu ya matini za kisheria.

#### **4.3 Sababu Zinazochangia Kutokea kwa Ukinzani wa Maana Kisheria Katiba Ilipotafsiriwa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili**

Tafsiri hufanywa ili kurahisisha kupitisha ujumbe kwa wasomaji ambao aghalabu huwa hawaelewi lugha iliyotumika kwenye MC. Tafsiri inapokuwa na utata basi maaana potovu huweza kuwafikia wasomaji na ujumbe ulionuiwa unakosa kuwafikia. Katika sehemu hii tuliangazia baadhi ya sababu ambazo zinachangia ukinzani wa maana kutokea wakati *Constitution of Kenya 2010* ilipotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Sababu hizi huweza kutokana na mtafsiri kutoelewa matini chanzi vizuri na

ukosefu wa istilahi za kisheria ambazo zinaweza kutumika badala ya kutumia maelezo. Tuliangazia baadhi ya sababu hizi katika sehemu ifuatayo.

Ukinzani wa maana umejitokeza kwa sababu ya tafsiri ya moja kwa moja ambayo imefanywa kwa kutozingatia muktadha wa kisheria. Kwa mfano katika Kifungu cha 24, ibara ya 1 (d); *Enjoyment of rights* imetafsiriwa kama *kufurahia wa haki hizo*. Tafsiri hii ni ya moja kwa moja kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. *Enjoyment* kwa Kiswahili ina maana ya *kufurahia*. Kisheria *enjoyment* ina maana ya kutekelezwa kwa haki bila kuwekewa kikwazo na mtu yeyote au kitu chochote. Tafsiri hii haikuzingatia kiwango cha usawidi wa kisheria na hivyo kukatokea ukinzani wa maana kisheria. Tafsiri iliyochukuliwa ni ile ya kawaida na hivyo kuzua tafsiri potovu.

Matumizi ya sentensi ndefu katika MC yamechangia kuwa na ukinzani wa maana kati ya MC na ML. Sentensi ndefu na changamano huzua utata wakati wa kutafsiri na hasa kwa mtafsiri kuzielewa na kuhawilisha mawazo yaliyomo hadi ML kwa ufasaha. Kulingana na Salmi-Tolonen (2004:1173), sentensi katika matini za kisheria huwa ndefu na huwa zinakidhi mahitaji tofauti. Sentensi hizi hutokea kwa sababu ya uchangamano wa maswala yanayojadiliwa katika tafsiri za kitaaluma. Sentensi hizi pia huwa na miundo tofauti kulingana na lugha inayotumika katika MC. Mtafsiri anapofuata muundo ule wa sentensi uliotumika katika MC basi ukinzani wa maana unatokea. Kwa mfano katika Kifungu cha 51, ibara ya (1);

**Kielelezo 56;**

Kifungu cha 51, ibara ya (1);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
51. (1) <b>A person</b> who is detained, held in custody or imprisoned under the law, retains all the rights and fundamental freedoms in the <b>Bill of Rights</b> , except to the extent that any particular right or a freedom is clearly incompatible with the fact that the person is <b>detained, held in custody or imprisoned</b> .	51. (1) <b>Mtu yeyote</b> anayezuiliwa kisheria, awe amehukumiwa au la, ana haki zote na uhuru wa kimsingi unaoelezwa kwenye <b>Katiba</b> hii, isipokuwa kwa kiwango kwamba haki au uhuru huo wa kimsingi hauambatani kabisa na sababu yake ya <b>kuwa kwenye jela</b> .

Urefu wa sentensi hii umezua changamoto katika kutafsiri. Tafsiri potovu inayojitokeza katika tafsiri hii ni kama vile, *a person* ambayo imetafsiriwa kama *mtu yeyote*, *Bill of Rights* imetafsiriwa kama *Katiba* na *detained, held in custody or imprisoned* inatafsiriwa kama *kuwa kwenye jela*.

Ukosefu wa istilahi mwafaka umechangia ukinzani wa maana kisheria MC inapotafsiriwa hadi ML. Matini za kisheria huwa na istilahi maalum ambazo hueleweka aghalabu na wale walio katika taaluma hiyo na kwa wasomaji wengine inabidi kurejelea walio na uelewa wa kisheria kupata maana au kurejelea vitabu vya kisheria. *Constitution of Kenya 2010* ina matumizi ya istilahi za kisheria ambazo zimezua changamoto wakati wa kutafsiri. Kwa mfano katika Kifungu cha 51, ibara ya (2), *habeas corpus* inatafsiriwa kama amri ya kufikishwa mahakamani. Maelezo ni ya kiisimu na wala hayaibui dhana ya kisheria. Hili linachangia kuwa na makala ambayo inakosa kuafiki kuwa ya kisheria kwani istilahi za kisheria hazitumiki. Mara nyingi katika tafsiri maelezo haya hutumika kwa sababu ya kukosa istilahi mwafaka katika ML ambayo inafiki ile iliyotumika kwenye MC.

Kuacha baadhi ya maneno au hata kuongezea maneno ambayo hayamo katika MC wakati wa kutafsiri pia kumechangia kutokea kwa ukinzani wa maana kati ya MC na ML. Katika kutafsiri sheria kila neno ni muhimu na kubadilishwa au kuongezwa kwa neno moja kunabadili maana ya kifungu kile. Kwa mfano;

**Kielelezo 57;**

Kifungu cha 40, ibara ya (3) (b) (i);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
40. (b) (i) <b>requires prompt</b> payment in full, of just compensation to the person; and	40. (b) (i) <b>inahakikisha</b> malipo kwa ukamilifu ya kumfidia mtu huyo <b>kabla ya mali hiyo kuchukuliwa;</b>

Katika kifungu hiki kwenye ML, kifungu '*kabla ya mali hiyo kuchukuliwa*' kimeongezwa na kuzua utata. Tafsiri hii haijatokana na maneno yoyote ambayo yamo katika MC. Katika utekelezwaji wa Katiba hii, hili linaweza kuleta utata na hivyo kubidi wahusika kurejelea MC ili kupata ufafanuzi sawa.

Kutozingatia urudiaji wakati wa kufanya tafsiri vilevile kumechangia kutokea kwa ukinzani wa maana. Sifa mojawapo ya sajili ya sheria ni kwamba huwa kuna urudiaji mwingi wa maneno na vifungu. Hili ni lazima pia lizingatiwe katika ML wakati wa kutafsiri. Kwa mfano;

**Kielelezo 58;**

Kifungu cha 19, ibara ya (3);

Constitution of Kenya 2010	Katiba ya Kenya 2010
19. (3) The rights and fundamental freedoms <b>in the Bill of Rights-</b>	19. (3) Haki na uhuru wa kimsingi <b>zinazotajwa katika sura hii-</b>

Katika mfano huu, kifungu *in the Bill of Rights* kinatafsiriwa kama *zinazotajwa katika sura hii*. Tafsiri hii ni potovu kwa sababu *in the Bill of Rights* inafaa kuwa *katika Sheria ya haki* kama ilivyotafsiriwa katika vifungu vingine. Tafsiri katika ML haijarudia kueleza sura hii inahusu nini bali imetaja huku ikichukuliwa kwamba msomaji anaelewa mada ya sura hii.

**4.4 Athari za Tafsiri Potovu kwa Watekelezaji wa Katiba**

House (1977), Reis (1989), na Lauscher (2000) walizua mikakati tofauti ya kuonyesha kile ambacho huchangia tafsiri bora na kama kweli tafsiri ile imekamilika au ina dosari. Ukinzani wa maana au tafsiri inapofanywa visivyo mara nyingi wasomi huichukulia ilivyo. Wasomi wengi huwa hawana muda wa kulinganisha MC na ML na kuona kama zina ujumbe sawa. Kutafsiri sheria hivyo basi kunahitaji mtafsiri awe makini sana ili kuwa na tafsiri bora na isiyo na ukinzani wowote wa kimaana. Tafsiri hizi zinapofanywa neno moja linaweza likabadilisha maana nzima ya makala inayotafsiriwa iwapo itatafsiriwa visivyo na ndiyo sababu kila neno ni lazima lizingatiwe wakati wa kutafsiri. *Katiba ya Kenya 2010* ina ukinzani wa maana unajitokeza wakati wa kutafsiri kama tulivyojadili na hili litakuwa na athari kwa watekelezaji wa Katiba hii. Raia kwa mfano anaweza kutia sahihi kwenye stakabadhi muhimu bila kuelewa maana yake.

Ukinzani wa kimaana katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* kunaleta ukosefu wa haki kwa watekelezaji wake. Kulingana na Molina Gutierrez (2002) tafsiri za kisheria huweza kuwa na athari za moja kwa moja kwa watekelezaji wake na kubadilisha maisha yao. Lugha ya kisheria huwa na majukumu muhimu ya kuhakikisha kuwa haki

imetendeka katika jamii. Lugha hii huwasilisha ujumbe unaohusiana na sheria na ambao unahitajika ili kuwa na jamii yenye utulivu na mpangilio. Tafsiri potovu kwenye Katiba basi inawasilisha ujumbe potovu kwa wananchi na ikija kwenye kutekelezwa kwake basi fasiri yake inaweza kuwa isiyofaa na kuishia kukosekana kwa haki.

Tafsiri potovu au yenye ukinzani na MC ina madhara hasa kwa watekelezaji wake kwa sababu hawataelewa ujumbe moja kwa moja. Hili litapelekea kupoteza muda mwingi sana hasa pale ambapo itabidi kutafuta wakili au yeyote aliye na fasiri ya vifungu vyenye utata. Kulingana na Tymoczko (2000), watu wengi hufanya tafsiri kwa sababu wanaamini kuwa watafaidi binadamu wengine au watakuwa na athari chanya kwa wanajamii. Ni muhimu basi kwa mtafsiri kufanya tafsiri isiyo na utata wa kimaana ili watekelezaji wake wapate ujumbe usiopotoka na wafaidike. Utata huu unaotokana na tafsiri utahitaji watekelezaji kurejelea MC ili kuelewa maana asili ya vifungu na istilahi tofauti.

#### **4.5 Mbinu Mwafaka Zinazoweza Kutumika Kutatua Ukinzani wa Maana**

Matumizi ya sentensi ndefu huzua utata wakati wa kutafsiri na tafsiri isipofanywa vizuri basi kunatokea ukinzani wa maana. Uelewa wa sintaksia ya lugha mbili zilizotumika katika kutafsiri Katiba ni muhimu sana. Mtafsiri anafaa kwanza achambue sentensi hii kwa kuzingatia muundo na kuelewa kwa kina ujumbe muhimu uliokusudiwa kupitishwa. Si lazima kutumia muundo wa sentensi uliotumika katika MC kwenye ML kwani kila lugha huwa na muundo tofauti wa sentensi. Kufuata muundo uliotumika katika MC kunaweza kuzua tafsiri potovu.

Ukosefu wa istilahi mwafaka za kisheria ambazo zinaweza kutumika katika ML unaweza kutatuliwa kwa njia mbalimbali. Kwanza, mtafsiri anaweza akaliacha neno jinsi lilivyo katika MC. Hili litatatua shida ya kutafuta neno linalofaa kutumika katika ML. Kwa mfano katika kifungu cha 51, ibara ya (2) *Habeas corpus* inatokana na lugha ya Kilatini na wala si maneno katika lugha ya Kiingereza lakini yametumika katika *Constitution of Kenya 2010*. Kanuni ya kutafsiri maneno ya kigeni sawia na haya inaeleza kwamba maneno hayo yanaweza kupotea katika matini lengwa lakini ni sharti maana yao iwasilishwe katika matini lengwa. Kwa mfano, *amicus curiae*—rafiki wa mahakama. Hii ina maana kwamba katika tafsiri ya Kiswahili inakubalika mtafsiri kuyaacha maneno

haya jinsi yalivyo kuliko kutumia maelezo ya kiisimu ambayo hayana maana yoyote ya kisheria. Inaruhusiwa pia kutumia utohozi pale ambapo hakuna istilahi mwafaka inayopatikana katika ML. Kwa mfano katika kifungu cha 54, ibara ya (1) (d), **Braille** imtafsiriwa kama **Breli**.

Tafsiri za kisheria huhitaji wataalamu wenye ujuzi na tajriba katika maswala ya kisheria. Kulingana na Cao (2014), maadili ni jambo muhimu kwa mtafsiri wa makala ya kisheria na kuwa na maadili ya hali ya juu kama mtafsiri ni ishara ya kukomaa na kuonyesha utaalamu katika kufanya tafsiri hiyo. Newmark (1988) anaeleza kuwa mtafsiri mzuri anafaa kuwa na uwezo wa kusoma na kuelewa MC hata kama imeandikwa kwa lugha geni na aelewe mada inayozungumziwa kwa kina.

Mtafsiri anafaa pia kuongozwa na nia ya tafsiri ile. Kulingana na nadharia ya *Skopos* tafsiri hufanywa kutegemea nia yake. Kwa mfano katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* mtafsiri alipaswa kuongozwa na dhana kwamba tafsiri hiyo ni ya kisheria na ni lazima lugha ya kisheria itumike. Hakuna vile misemo au nahau ingetumika katika Katiba kwa sababu hii ni makala ya kipekee na yenye urasmi. Iwapo mtafsiri atakosa kuongozwa na nia ya tafsiri ile basi kutatokea tafsiri potovu. Ni muhimu pia mtafsiri awe na mikakati aliyoweka ili kumwongoza kufikia nia ile.

Tafsiri itazidisha ubora wake ikiwa imesomwa na kurudiwa mara kadhaa ili kurekebishwa na kuondoa makosa yaliyopo. Kurekebishwa huku kunaweza kufanywa kwa kusoma MC na kuona kama maana iliyokusudiwa imehawilishwa hadi ML na pia kwa kutafsiri tena ML hadi MC na kuona kama maana ile itabakia. Watu mbalimbali wanaweza kutumika ili kupitia makala ile na kuwasilisha maoni yao. Mtafsiri anaweza pia kutumia makala nyingine ya kisheria iliyotafsiriwa ili imwongoze katika kufanya tafsiri yake ingawaje hili linafaa kufanywa kwa uangalifu lisilete utata. Ili kutekeleza haya yote muda wa kutosha utahitajika. Haya yote yakifuatwa basi tafsiri itakuwa yenye ubora zaidi.

#### **4.6 Hitimisho**

Kutokana na mijadala ambayo tuliifanya katika sura hii, kuna dosari, makosa, kasoro na upotoshi wa maana za kiisimu na kisheria ambao umejitokeza kutokana na kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* hadi Kiswahili kama *Katiba ya Kenya 2010*, zimetokana na udhibiti dhaifu wa maana za kisheria, ukosefu wa istilahi za kisheria katika lugha ya Kiswahili, udhaifu wa kudhibiti na kuwa na uelewa wa wasifu wa usawidi wa kisheria, upuuzaji kanuni za kisheria kama vile matumizi ya sentensi ndefu.

## **SURA YA TANO**

### **MUHTASARI, MAHITIMISHO NA MAPENDEKEZO**

#### **5.0 Utangulizi**

Sura hii inatoa muhtasari wa utafiti wetu kuhusiana na ukinzani wa maana kisheria kwenye *Katiba ya Kenya 2010*. Tumeeleza kuhusiana na mafanikio katika utafiti huu na kuonyesha changamoto tulizokumbana nazo wakati wa kufanya utafiti huu. Baadaye tumetoa maoni yetu kuhusiana na utafiti huu na kutoa mapendekezo zaidi ambayo yanaweza kufanywa ili kuchangia zaidi katika tafsiri zinazohusiana na taaluma ya kisheria.

Katika utafiti huu tulilenga kubaini kama kuna ukinzani wa maana uliojitokeza wakati wa kutafsiri MC (*Constitution of Kenya 2010*) hadi ML (*Katiba ya Kenya 2010*). Tuliangazia pia sababu ambazo zinaweza kuwa zilichangia ukinzani huu, athari za ukinzani huu kwa wapokezi na mbinu mwafaka zinazoweza kutumika kutatua ukinzani huu. Tulikusanya data kutoka kwenye Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010* (makala ya Kiingereza na Kiswahili). Katiba nzima ingawaje ilitusaidia kwenye utafiti huu ili kuelewa baadhi ya sifa za matini za kisheria. Kwa sababu ya muda hatungeweza kungazia Katiba nzima. Sura tulizochagua pia zilikidhi mahitaji ya utafiti huu kwa kiwango kikubwa tukilinganisha na sura zile zingine. Tuliongozwa na nadharia ya *Skopos* inayolenga hasa nia katika tafsiri.

Katika sura ya pili tumeeleza kuhusiana na sajili ya kisheria kwa kijumla na changamoto katika kuitafsiri. Tumeonyesha kuwa tafsiri za kisheria ni za kipekee na zinahitaji mtafsiri awe makini na mwangalifu wakati wa anapotafsiri. Tumeanza kwa kuelezea kuhusu wasifu wa sajili ya kisheria kwa kijumla. Kisha tumeangazia tumefafanua sifa za Katiba kama matini ya kisheria. Mwishowe tumeshughulikia changamoto ambazo hujitokeza wakati wa kutafsiri hasa kwa kugemea upande wa kisheria na tukaonyesha jinsi tunaweza kukabiliana na changamoto hizi.

Katika sura ya tatu, tumeangazia Sura ya 3 ya *Constitution of Kenya 2010* na kuelezea kwa muhtasari mambo muhimu yaliyojitokeza katika hii. Baadaye tumeiwasilisha data kutoka kwenye MC (*Constitution of Kenya 2010*) kwenye jedwali na kuilinganisha na ile katika ML (*Katiba ya Kenya 2010*). Tumefanya hivi kwa kuweka kila data muhimu



katika MC ikilingana moja kwa moja na ile ya ML. Tumekoleza kwa wino mzito data ambayo inazua maana kinzani katika vifungu vyote. Kisha tumefanya mjadala kuonyesha ukinzani wa kimaana unaojitokeza katika Sura ya 3.

Katika sura ya 4 tumechanganua data kutoka kwenye Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010* na kuchunguza ukinzani wa kimaana unaojitokeza hasa sura hii inapotafsiriwa kutoka MC hadi ML. Katika uchanganuzi wetu tumeongozwa na malengo ya utafiti huu na nadharia ya *Skopos*. Tumeeleza pia sababu ambazo zinaweza kuwa zilichangia kutokea kwa ukinzani huu wa kimaana. Baadaye tumeangazia athari za tafsiri potovu katika uwasilishaji wa maana hasa kwa wapokezi wake na kisha tukajadili mbinu mwafaka za kutatua ukinzani huu.

### **5.1 Mafanikio, Maoni na Mapendekezo**

Katika utafiti huu tulinuia kuonyesha mkinzano wa maana za kiisimu na za kisheria unaojitokeza wakati wa kutafsiri istilahi na Vifungu vya *Constitution of Kenya 2010* kutoka MC hadi ML. Tulilenga Sura ya 3 na Sura ya 4 ya *Constitution of Kenya 2010*. Sura ya 3 inahusu Uraia ilhali Sura ya 4 inahusu Sheria ya Haki. Tumefanikiwa kuonyesha ukinzani huu wa maana unavyojitokeza na jinsi ya kuutatua kama vile tumeonyesha katika uchanganuzi wa data.

Kufanya utafiti huu haikuwa jambo rahisi kutokana na istilahi za kisheria ambazo ni ngumu kuelewa. Inahitaji mtu kuwa na uelewa wa kisheria ili kuelewa vizuri jinsi ya kutafsiri Katiba na pia kuwarejelea wenye ujuzi huu. Vitabu na makala yaliyopo yameandikwa kwa lugha ya Kiingereza na pia kuyatafsiri haikuwa jambo rahisi. Makala ambayo yanahusu tafsiri za kisheria kwa lugha ya Kiswahili ni chache mno. Katika utafiti wetu basi ilitubidi kujikakamua kwa sababu hatukuwa na ujuzi wa hali ya juu kuhusu maswala ya kisheria. Mwishowe tumeishia kujifunza mengi yanayohusiana na taaluma hii.

Utafiti huu ulijishughulisha na ukinzani wa maana kisheria unaojitokeza katika kutafsiri *Constitution of Kenya 2010* kutoka lugha ya Kiingereza hadi lugha ya Kiswahili. Kulingana na maoni yetu ni kwamba mtafsiri inafaa aelewe kwamba matini za kisheria ni za kipekee ikilinganishwa na nyanja zingine na hivyo zinahitaji mwelekeo mahususi na

tofauti katika kuzitafsiri. Kila matini hutafsiriwa kwa kutumia mwelekeo tofauti kutegemea lengo au nia. Mtaalamu wa tafsiri inabidi pia asitumie kamusi moja pekee katika kutafsiri kwake. Ingawaje kamusi hizi husaidia wakati wa kutafsiri zinafaa zitumike kwa uangalifu sana huku akinuia kulenga maana inayokusudiwa na si kuchukua maana ya kamusi pekee bila kuihusisha na maana ya kisheria.

Mwishowe baada ya kutafsiri, matini lengwa lazima ihaririwe kwa kina zaidi kuhakikisha kuwa imetafsiriwa ipasavyo. Mtaalamu hufanya hivi ili kuhakikisha kuwa ujumbe ulionuiwa kupitishwa umefanywa hivi kutoka matini chanzi hadi matini lengwa bila kupoteza maana. Anapopitia kazi yake, yeye pia huweza kutoa makosa ambayo huenda yalifanyika wakati wa kutafsiri. Lazima mtaalamu ahakikishe kuna mtiririko wakati wa kutafsiri na si kutafsiri neno moja kwa moja bila kuzingatia muktadha. Pia ahakikishe kuwa Katiba inapotafsiriwa haijapoteza urasmi wake kama makala ya kisheria.

Katika utafiti huu tulifanikiwa katika kuyajibu maswali ya utafiti ambayo tulikuwa nayo. Kuna mambo mengi ambayo tungeweza kushughulikia katika sura hizi lakini kutokana na upeo na mipaka katika utafiti huu hatungeweza. Tuliangazia sura mbili pekee kutokana na Sura 18 za *Constitution of Kenya 2010*. Tunapendekeza kuwa tafiti zaidi zifanyike kuhusu sura zilizobakia na aina nyinginezo za matini za kisheria ambazo hazijashughulikiwa ili kuchangia katika uwanja huu. Tafiti nyingi ambazo zimefanywa zinahusu tafsiri za fasihi andishi kama vile riwaya, ushairi na tamthilia. Hivyo basi kuna haja ya kufanya tafiti zinazohusiana na sheria.

## **MAREJELEO**

Austin, J. L. (1962). *How to do Things with Words*. The Clarendon Press: Oxford.

Cao, D. (2007). *Translating Law*. Amazon: Multilingual Matters.

\_\_\_\_\_ (2014). *Afterword: The Trials and Tribulations of Legal Translation*. In L: Cheng, K.

Crystal & Davy (1969). *Investigating English Style*. Indiana University Press.

Endicott & Timothy A. O. (2000). *Vagueness in Law*. Oxford: Engberg, Jan. 2004. *Statutory Texts as Instances of Language(s): Consequences and Limitations on Interpretation*. Brooklyn.

Gentzler, E. (2001). *Contemporary Translation Theories*. New York: Routledge

Hart, H. L. A. (1954). "Definition and Theory in Jurisprudence." *Law Quarterly Review*, 70: 37–60.

Halliday, M. A. K. (1984) 'Language as Code and Language as Behaviour: A Systemic-functional Interpretation of the Nature and Ontogenesis of Dialogue'. Robin Fawcett, MAK.

Harvey, M. (2002): *What's so Special About Legal Translation?* Meta.

Hilf, M. (1973). *Die Auslegung mehrsprachiger Verträge [The Interpretation of Multilingual Treaties]*. Heidelberg, Germany: Springer.

House, J. (1977). *A Model for Translation Quality Assessment*. Tübingen: Narr.

<http://www.citeulike.org/group/740/author/Nida:EA>

Jowitt E. & Walsh C. (1959). *The Dictionary of English Law*. New Fetter Lane London: Law Publishers.

*Katiba Inayopendekezwa ya Kenya*, (2010). Mwanasheria Mkuu, Government Press.

- Lauscher, S. (2000), "Translation Quality Assessment: Where Can Theory and Practice Meet?" In: The Translator. *Studies in Intercultural Communication*. Evaluation and Translation, Volume 6, Number 2, 2000. Manchester, U.K.: St. Jerome Publishing, pp. 149-168.
- Kui Sin & Wagner, A. (Eds.). *The Ashgate A Handbook of Legal Translation* (pp. 313–315). Farnham. UK: Ashgate.
- Mlacha S.A.K. (1999). *Kamusi ya Sheria Kiingereza – Kiswahili*. TUKI: Dar es Salaam.
- Mellinkoff, D. (1963). *The Language of the Law*. Eugene: Resource Publications.
- Molina Gutiérrez, M. (2002). *Análisis Funcionalista del Formulario de Solicitud del Visado de Schengen [A Functionalist Analysis of the Schengen visa Application]*. Puentes, 2, 55–65. Retrieved from <http://www.ugr.es/~greti/puentes/puentes7/06-Molina-Gutierrez.pdf>
- Mwansoko, H. J. M, and Tumbo-Masabo, Z. N. Z. (1992). *Kiongozi cha Uundaji Istilahi za Kiswahili*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.
- Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation*. New York: Prentice-Hall.
- \_\_\_\_\_ (2005). *A Textbook of Translation*. London: Longman.
- Nijamp, P, Rietveld P, & Salomon, I. (1990). *Barriers in Spatial Interactions and Communications*. Aconceptual exploration. *Ann Reg Sci* 24:237 -252
- Nord, C. (1997). *Translating as a Purposeful Activity*. Manchester: St. Jerome
- Penner, J. E. (2001). *Mozley and Whiteley's Law Dictionary*. London: Butterworths Publishers,
- Pommer, S.E. 2008. *No Creativity in Legal Translation?* *Babel*, 54(4):355-368.

- Reiss, K 1989. “*Text Types, Translation Types and Translation Assessment*”. Trans, by Andrew Chestennan, (ed.), pp. 105-115.
- Sakareva, I. (2001, September) *Difficulties & some problems in Translating Legal Documents*, 133-138. Retrieved from <http://www.google.com/gwtlx?wsc>.
- Salmi-Tolonen, Tarja (2004): “*Legal Linguistic Knowledge and Creating and Interpreting Law in Multilingual Environments*”. *Brooklyn Journal of International Law* [vol. 29:3], 1167-1191.
- Šarčević, S. (1988): *Bilingual and Multilingual Legal Dictionaries: New Standards for the Future*, Meta.
- Šarčević, S. (1989): *Conceptual Dictionaries for Translation in the Field of Law*, *International Journal of Lexicography*.
- Sarcevic, S. 1997. *New Approach to Legal Translation*. The Hague: Kluwer Law International.
- Schäffner, C. (1998). From “good” to “*Functionally Appropriate*”: *Assessing Translation Quality*. In C. Schäffner (Ed.), *Translation and quality* (pp.1–5). Clevedon, UK: Multilingual Matters.
- Schaffner, C. (1998). *Current Issues in Language and Society*, citeulike.org.
- Shiflett, M. (2012). *English Matters, Functional Equivalence and its Role in Legal Translation*; Prešov University.
- Soriano Barabino, G. (2006). *Los Retos de la Traducción Jurídica en el Siglo XXI [The Challenges for Legal Translation in the 21st Century]*. In *Traducción, Lengua y Cultura en los Albores del Siglo XXI [Translation, Language and Culture on the Verge of the 21st Century]* (pp. 287–297). Granada, Spain: Jizo Ediciones.
- The Constitution of Kenya*, 2010. Nairobi, Government Printer.
- Toury, G. (1995). *Descriptive Translation Studies*. Amsterdam: John Benjamins.

- Tymoczko, M. (2000). *Translation and Political Engagement: Activism, Social Change and the Role of Translation in Geopolitical Shifts*. *The Translator*,6(1), 23–47.
- Vermeer, H. (1989a). ‘*Skopos and Commission in Translational Action*’ katika Chesterman, A (Ed). *Readings in Translation Theory*. Pp 99-104.
- Waithira, N. G. (2014). *Changamoto za Kutafsiri Matini za Kisheria: Tathmini ya Katiba ya Kenya* (2010).
- Way, C. (2002). *Traducción y Derecho: Iniciativas para Desarrollar la Dolaboración Interdisciplinar* [*Translation and Law: Initiatives for Interdisciplinary cooperation*]. *Puentes*, 2, 15–26.
- Weston, M. (1991). *An English Readers Guide to the French Legal System*. New York: Oxford. Berg.
- Wydick, Richard C. (1998). *Plain English for Lawyers*. Durham, N.C.: Carolina: Academic Press.
- Zaja, J. O. (2018). *Translating the Constitution of Kenya, 2010: The Illusion and Veracity of a Linguistic Trajectory in the Translation of Legal Texts with Special Reference to Chapter 11*. *Mara res. j. humanities soc. sci.* Vol. 3, No. 2, Pages 21 - 87, ISSN: 2519-1489